Nipashe
Alhamisi Februari 11, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580488
www.ippmedia.com
The Guardian digital   nipasheTZ   nipasheTZ   nipasheTZ   0745 700710




UKURASA 11

**SERIKALI** yaeleza sababu kufuta Nanenane mwaka huu

UKURASA 2



**WANAFUNZI** 7,400 bado hawajaripoti kidato cha kwanza

UKURASA 3

# Vifo vigogo vyazua hofu

UK. 2



Wakili Geofrey Noah



Arcado Ntagazwa



Wakili Samuel Mwamgiga



Mhandisi Robert Marealle



Dk. Ambwene Mwakyusa

## GWAJIMA AWARUKIA WANAOMBEZA MAGUFULI

UKURASA 3

# Rais akemea walioeneza ugonjwa wa Maalim Seif

UKURASA 2,4

**MICHEZO** **AS VITA YAITISHA SIMBA** UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6

# Vifo vya vigogo vyazua hofu

**Na Mwandishi Wetu**

NI hofu na taharuki. Ndivyo inavyoweza kuelezewa kutokana na vifo vya ghafla vya watu mashuhuri wakiwamo wafanyabiashara na waliowahi kushika nyadhifa mbalimbali serikalini.

Vifo hivyo ni mfululizo wa matukio ya watu mbalimbali kupoteza maisha ndani ya wiki kadhaa sasa wakiwamo wanataaluma nguli katika taasisi za elimu ya juu pamoja na viongozi wa dini.

Ndani ya siku tatu, kwa mfano, watu kadhaa wenye majina makubwa wamefariki dunia huku jana taarifa zikitolewa kuwa aliyewahi kuwa Waziri katika serikali ya awamu ya kwanza, ya pili na ya tatu, Arcado Ntagazwa, akiwa mmojawapo.

Taarifa hizo zilibainisha kwamba Ntagzwa, ambaye mwaka 2015 alijiengua Chama Cha Mapinduzi (CCM), alifariki dunia usiku wa kuamkia jana katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Mloganzila, alikokuwa amelazwa kwa matibabu.

Ntagazwa (75) ambaye hadi kufariki dunia kwake alikuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Mwanasiasa huyo nguli ambaye kitaaluma alikuwa mwanasheria, baada ya kumaliza chuo kikuu, alifanya kazi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Waziri Mkuu, Idara ya Usalama wa Taifa.

Aliingia katika siasa mwaka 1980 akiwa Mbunge wa Jimbo la Kibondo na kushika nafasi za unaibu waziri na uwaziri katika serikali za awamu ya kwanza, ya pili na ya tatu hadi mwaka 2005 alipoangushwa ubunge na Felix Kijiko katika Jimbo la Muhambwe.

Katika serikali ya awamu ya kwanza, aliwahi kuwa Naibu Waziri wa Fedha (1983-85) na baadaye Wizara ya Mawasiliano, Uchukuzi na Ujenzi (1986-87).

Baada ya hapo alipandishwa na kuwa Waziri wa Ardhi, Maliasili na Utalii nafasi ambayo aliishika hadi Machi 1990 baada ya Rais wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, kuvunja Baraza la Mawaziri.

Mwaka 2000, wakati wa utawala wa awamu ya tatu chini ya Rais Benjamin Mkapa, Ntagazwa aliteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) hadi mwaka 2005.

Mbali na Ntagazwa, mtu mwingine mashuhuri aliyefariki dunia ni Mkurugenzi wa Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), Daniel Loya. Loya alifariki dunia jana katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) wakati akiendelea na matibabu ya maradhi yaliyokuwa yakimkabili.

Taarifa zaidi zilizopatikana jana ni pamoja na kifo cha Sadala Ndossi, mmiliki wa kampuni ya Saba General Enterprises, inayojishughulikisha na masuala ya uuzaji wa spea za magari, milki na vifaa vya ujenzi.

Ndossi, mfanyabiashara maarufu Dar es Salaam na Arusha, alifariki dunia jana katika Hospitali ya Muhimbili.

Mwanasiasa mkongwe, msomi na aliyekuwa Waziri katika serikali ya awamu ya tatu na ya nne, Prof. Mark Mwandosya katika ukurasa wake wa twitter aliandika kuhusu kifo cha Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Wasanifu Majengo Tanzania (AQSRB), Dk. Ambwene Mwakyusa.

Katika taarifa hiyo, Prof. Mwandosya aliandika kuwa mtaalamu huyo amefariki dunia baada ya kuugua muda mfupi.

Kama vile haitoshi, taarifa za kushtua zilitua katika tasnia ya sheria baada ya kutangazwa vifo vya mawakili wawili maarufu. Mawakili hao si wengine bali ni Samuel Mwamgiga aliyekuwa anafanya shughuli zake Iringa na Geofrey Noah wa Arusha.

Mtoto wa Mwamgiga, Wakili Jessy, alikaririwa na vyombo vya habari akisema baba yake alikuwa akisumbuliwa na maradhi kwa wiki mbili na jana asubuhi alifariki dunia na kwamba msiba uko Mkimbizi Shayo na taratibu za mazishi zilikuwa zinafanyika.

Wakili Noah kwa upande wake, alifariki dunia katika Hospitali ya Selian ya jijini Arusha, wakati akiendelea na matibabu.

Taarifa zaidi zilizolifikia gazeti hili zilibainisha kuwa mfanyabiashara maarufu, Humphrey Luwanja, alifariki dunia usiku wa kuamkia jana baada ya kuzidiwa ghafla kutokana na maradhi yaliyokuwa yakimsumbua kwa muda mrefu.

Luwanja ambaye aliwahi kuwa mmiliki wa Hoteli ya Village Motel na baadaye Shule ya Sekondari ya Midland zote za jijini Dar es Salaam, anatarajiwa kuzikwa kesho kutwa katika makaburi ya Kinondoni.

# Mwinyi akemea walioeneza ugonjwa wa Maalim Seif

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amekemea tabia ya kutangaza ugonjwa unaowakabili watu, akisisitiza kuwa amewashangaa waliotangaza ugonjwa anaougua Makamu wa Kwanza Rais, Maalim Seif Sharif Hamad.

Amesema kamwe hatatangaza hali ya kiafya ya Maalim Seif kwa sababu kutangaza ugonjwa wa mtu bila ridhaa yake, ni kwenda kinyume cha maadili ya taaluma ya udaktari.



Dk. Mwinyi ambaye kitaaluma ni tabibu, alitoa kauli hiyo juzi jioni Ikulu mjini Unguja, alipoulizwa swali na waandishi wa habari kuhusu hali ya kiafya ya kiongozi mwenzake huyo.

Katika majibu yake, Rais Mwinyi alisema maadili ya kidaktari hayaruhusu kutangaza ugonjwa wa mtu hadharani, akisisitiza waliofanya hivyo, wamekosea.

"Suala la ugonjwa wa mtu ni kazi ya daktari wake na mgonjwa mwenyewe. Sipo tayari kutangaza ugonjwa wa mtu," Rais Mwinyi alisema.


Alisema kukitokea nafasi ya kutoa taarifa, wahusika watatoa taarifa na siyo yeye kwa kuwa kitaaluma, haifai kutoa taarifa za mgonjwa.

Katika mkutano wake huo, Rais Mwinyi pia aliulizwa kuhusu baadhi ya watu kuhodhi ardhi visiwani Zanzibar, akisema kuwa tayari ameshatoa maagizo kwa watu wote waliojigawia ardhi washughulikiwe.

Alisema kuwa siyo sahihi wananchi kukosa ardhi huku watu wachache hasa viongozi wa serikali, wamehodhi maeneo makubwa.

"Nimepewa taarifa kwamba wakati sisi tuko 'busy' na kampeni, kuna baadhi ya viongozi walikuwa 'busy' kugawana ardhi. Nimeagiza maeneo yote yaliyogawiwa, yarejeshwe serikalini na utaratibu uliotumika ufutwe. Siyo sahihi wananchi kukosa ardhi na kujigawia wao," alionya.

Dk. Mwinyi pia alisifu viongozi wa upinzani, hususan Chama cha ACT-Wazalendo, kwa kukubali kuungana naye kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar "bila kuwapo wapatanishi kutoka nje ya nchi".




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KISUTU
DAR ES SALAAM

SHAURI LA MADAI NO. 96 YA 2018

THE CONTRACTORS REGISTRATION BOARD .................. MDAI

DHIDI YA

M/S RANKY INFRASTRUCTURE & ENGINEERING LTD .......... MDAIWA

KWA: Managing Director,
M/S Ranky Infrastructure & Engineering Ltd
**Dar es Salaam**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya Mdai yameelezwa katika nakala ya madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo Unahitajiwa kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au kwa Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa, siku ya tarehe **15/02/2021** Saa **7:00** Mchana. Kwa mujibu wa madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutajwa shauri hilo ni lazima mlete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

**ANGALIA:**
Kama hautahudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea Kuitwa Shaurini, itaweza kusikiliza bila wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo tarehe **26** Mwezi wa **JANUARY, 2021**

**HAKIMU MKAZI MKUU**
**KISUTU - DAR ES SALAAM**


## Sababu za Nanenane kufutwa mwaka huu

**Na Renatha Msungu,**

DODOMA

SERIKALI imefuta maonyesho ya Nanenane kwa mwaka 2021, badala yake fedha zilizotengwa kwa ajili ya maandalizi hayo zitaelekezwa katika kuimarisha shughuli za ugani kwenye sekta ya kilimo.

Uamuzi huo ulitangazwa jana na Waziri wa Kilimo, Prof. Aldof Mkenda, akisema umetokana na majadiliano na maazimio ya kikao cha siku mbili cha maofisa kilimo wa mikoa, wilaya na halmashauri nchini ambapo walielezea changamoto mbalimbali wanazokutana nazo ambazo zinahitajika kutatuliwa.

"Katika kikao hicho, maofisa hao walieleza changamoto mbalimbali ambazo ni muhimu zipatiwe ufumbuzi ndipo tukaazimia kufuta maonyesho hayo ili fedha za maandalizi zielekezwe katika shughuli za ugavi," alisema Prof. Mkenda.

Ingawa hakutaja kiasi cha fedha hizo, alisema wameunda kikosi maalumu (task force) kufanya tathmini kuona kama maonyesho hayo yanaleta tija ikiwamo kuyaboresha kwa kuzingatia kuwa yanakwenda sambamba na shughuli za kilimo.

Aliwataka watendaji wote ambao tayari wameanza kuchukua posho kwa ajili ya kuhudhuria vikao mbalimbali vya maandalizi kusitisha mpango huo, huku akiagiza wale walioko njiani kuelekea Tabora kwa ajili ya maandalizi ya maonyesho hayo kusitisha shughuli hizo haraka iwezekanavyo.

"Nafahamu kuna watu wameanza maandalizi ya maonyesho hayo, na wengine wanajiandaa kuelekea Tabora, naomba watendaji kusitisha vikao vyote vya maandalizi, ikiwamo kuacha kuchukua posho inayohusiana na maandalizi ya kazi hiyo," alisema Prof. Mkenda.

HABARI KITAIFA

# Wanafunzi 7,400 waliochaguliwa hawajaripoti kidato cha kwanza

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAFUNZI 7,416 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2021 mkoani hapa, hawajaripoti shuleni.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Albert Msovela, alitoa taarifa hiyo jana kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) mjini hapa.

Alisema katika mkoa huo, wanafunzi 26,217 walichaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu, wakiwamo wavulana 12,360, wasichana 13,857, lakini walioripoti shuleni ni 19,776 ambao ni wavulana 9,718, na wasichana 10,058.

"Natumia fursa ya mkutano huu kutoa wito kwa wakurugenzi wa halmashauri, maofisa elimu na watendaji wengine wa serikali kuhakikisha ifikapo mwezi ujao, niwe nimepata taarifa za wanafunzi hawa 7,416 ambao hawajaripoti shuleni," alisema Msovela.

Pia aliwaagiza wakuu wa wilaya na wakurugenzi kuhakikisha wanasimamia vyema ujenzi wa vyumba vya madarasa, ili agizo la Waziri Mkuu la kutaka kukamilisha ujenzi wa madarasa kabla ya kufikia Februari 28, mwaka huu.

Katika hatua nyingine, Msovela aliwataka wadau wa maendeleo mkoani humo kujitokeza kuchangia viti, meza pamoja na madawati ili wanafunzi wasikae chini.

Kaimu Ofisa Elimu Mkoa wa Shinyanga, James Malima, alisema mpaka sasa mkoa huo unakabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa 142 kwa shule za sekondari.

# Gwajima: Wanaopinga miradi ya JPM wagonjwa

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MBUNGE wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima (CCM), amedai watu wanaopinga utekelezaji wa miradi mikubwa na maendeleo yaliyopatikana wakati wa awamu ya Rais Dk. John Magufuli ni wagonjwa.

Akichangia bungeni jana mjadala wa mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango, Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2021/22 na Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano wa mwaka 2021/22 -2025/26, Gwajima alisema watu hao wanaugua ugonjwa usiotibika unaoitwa 'Schizophrenia'.

"Kumekuwa na hoja zinazozungumzwa hapa bungeni, kuonyesha kwamba awamu ya Rais Magufuli haijafanya jambo lolote. Mheshimiwa Spika, mimi nasema mtu ambaye haamini hilo, ana ugonjwa hatari usiotibika nchini. Asiyeona ana ugonjwa wa Schizophrenia (tatizo la afya ya akili)," alisema Askofu Gwajima, mkuu wa Kanisa la Ufufuo na Uzima.

Alidai watu hao wanaopinga miradi na maendeleo yaliyofanywa na Rais Magufuli wana ugonjwa maalumu unaohitaji tiba maalumu.

Alisema kuanzia mwaka 1976 hadi 1981, kulikuwa na ndege 11 na hadi nchi inaingia kwenye hatua ya ubinafsishaji kulikuwa na ndege tisa na Rais Magufuli alivyoingia madarakani mwaka 2015, hapakuwapo na ndege, lakini ndani ya kipindi cha miaka mitano, Tanzania ina jumla ya ndege 12.

"Mheshimiwa Naibu Spika, unakumbuka vizuri Shirika la TANESCO, kabla ya JPM (Rais Magufuli) hajaingia madarakani lilikuwa linaendeshwa kwa kupewa ruzuku ya Sh. bilioni 438 kila mwaka, lakini tangu mwaka 2015, linajiendesha lenyewe kwa fedha yake yenyewe na linafanya vizuri, asiyeona ana ugonjwa maalum unahitaji daktari maalumu," alisema.

Alisema pia mwaka 2015, Tanzania ilikuwa na vijiji 2018 vilivyokuwa na umeme, lakini ndani ya miaka mitano vijiji 10,263 vina umeme.

"Na kwa taarifa ya asiyeona (wanaopinga) ni kwamba vimebaki vijiji 2,005 tu kwa Tanzania yote iwe na umeme. Na ni muhimu kujua pamoja na mambo mengine yote mwenye macho ni muhimu atazame wapi tunatoka na wapi tunapoelekea kwa sasa. "Sikiliza niwaambie tangu Tanzania ianze enzi za ma-rais waliopita ilikuwa na megawati za umeme 1,602 lakini sasa kupitia mradi huo wa Mwalimu Nyerere pekee yake utazalisha umeme wa megawati 2,115. Sasa utaachaje kuongea kuhusu huu mradi?" Alihoji.

Vilevile, alisema akiwa nchini Japan, alishuhudia nchi hiyo ikiwa na treni ya umeme yenye kasi ya kilomita 250 kwa saa, pamoja na treni nyingine itakayozinduliwa hivi karibuni inayopita ardhini itakayokuwa na kasi ya kilomita 500 kwa saa.

"Sisi hapa Tanzania kwa upande wa Afrika Mashariki, tumekuwa nchi ya kwanza kutekeleza mradi wa treni yenye uwezo wa kwenda kilomita 160 kwa saa, utasemaje JPM (Rais Magufuli) hajafanya vitu vyake, unahitaji dawa maalumu na daktari maalumu kusema hivyo," alisisitiza.

Alisema wakati Rais Magufuli anaingia madarakani tembo nchini walikuwa wamebaki 15,000, lakini ndani ya uongozi wake wa miaka mitano, leo kwa mujibu wa taarifa za Wizara ya Maliasili na Utalii, wapo tembo 60,000 na wanazaliana bila utaratibu.

Kuhusu sekta ya afya, alisema kipindi cha uhuru nchi ilikuwa na hospitali za wilaya 77, lakini ndani ya miaka mitano ya Dk. Magufuli, sasa zimejengwa hospitali 102.

"Tulikuwa na Hospitali za Rufani za mikoa 18 tangu Uhuru, lakini ndani ya miaka mitano zimejengwa 10, asiyeona ana ugonjwa wa Schizophrenia," alisisitiza.

VisionFund TANZANIA

**VISIONFUND TANZANIA MICROFINANCE BANK LTD**

**VACANCIES**

VisionFund Tanzania Microfinance Bank Ltd (VFT MFB) formerly known as SEDA is a fast growing and reputable Micro Finance Bank (MFB), has a loan book of TZs. 17 billion and 30,000 customer base, more that 5,000 of them being small holder farmers. VFT-MFB is seeking to employ a dynamic and committed Tanzanian young men & women who have passion for people's economic development to fill in the vacant positions detailed here below;

**Work reference no. 001**
**Position: Senior People and Culture Officer**
**Reporting to: Head of People and Culture (HPC)**

**Responsibility:**

. Responsible for Assisting/ supporting the Head People and Culture in facilitating all personnel related issues (recruitment, training, talent management & performance management) in accordance with VFT - MFB's policies

**Main tasks**

1. Prepare and update manpower plan and succession plan.
2. Responsible for recruitment, advise the HPC on shortlisted candidates to ensure that the organization has the required quality of staff.
3. Prepare P & C budget for Board approval.
4. Prepare and update Compensation and Package Scheme.
5. Work with HPC to prepare position matrices for staff and design staff positions and HAY grades in accordance with the organization changes.
6. Monitor report and suggest appropriate actions with regards to staff turnover.
7. Responsible for P&C/HR manual review.
8. Ensure annual staff training plan & budget.
9. In collaboration with HoD develops and reviews staff update/training manuals/modules.
10. Work with the HPC to coordinate Our Voice survey & reporting, monitor the implementation of the identified gaps.
11. Ensure consistent coaching for performance conversations.
12. Monitor all employment contracts and ensure timely update of staff contract in accordance to the country labor laws.
13. Keep track on all legal issues in liaison with Advocates and Department/ Business Centre & Branch Managers on matters arising from different areas of operations.
14. Provide guidance to the P&C whistleblower committee on policies & regulations governing staff disciplinary and other related matters.
15. Responsible for Staff Monthly reports and newsletters when due.
16. Respond to daily employees' questions/issues timely and in an appropriate manner.

**Education/Experience**

. Bachelor Degree in Human Resources Management
. At least 5 years' experience in a professional HR environment
. Understanding and training in the Labour laws in Tanzania
. Experience with and proficiently in using Human resource information systems
. Payroll management and experience in benefits administration is preferred

**Special / Personal Abilities**

. Highly developed sense of reliability and correctness
. Excellent trainer, facilitator, mentor and coach
. Innovative and analytical
. Very good planning skills
. Proficient in Micro Soft office applications
. Must be a self-starter, highly motivated, organized, and detail-oriented
. Model and demonstrates effective Christianleadership

About our working environment & remuneration.
VisionFund Tanzania Microfinance Bank has a calm and harmonious working environment where staffs are highly valued. Good work is recognized and rewarded accordingly and there is an opportunity to grow professionally and spiritually.

**Mode of Application:**
Interested and suitably qualified individuals should forward their application letter, attaching copies of their academic and professional certificates; detailed CV's with three referees to vftHRstaff@vftz.co.tz.The position should be the subject of the email application. OR through the postal address below.

**The Chief Executive Officer, VisionFund Tanzania Microfinance Bank Limited**

**P.O. Box 1546, Arusha TANZANIA.**
**The application should reach the undersigned not later than 24th February 2021.**

**N.B. Only short-listed candidates will be contacted**

**Disclaimer**
VisionFund Tanzania Microfinance Bank would like to inform the general public that it has not engaged any consultant/agent to conduct recruitment on its behalf

## MAHOJIANO MAALUM -3

# Mwinyi: Kesi za ukatili zitaondolewa dhamana

**Na Sanula Athanas,** ZANZIBAR

KATIKA sehemu ya pili jana, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alifafanua mikakati ya serikali yake kupunguza alichokiita utitiri wa kodi na namna watakavyoendeleza uwekezaji na kuwezesha biashara.

Katika mwendelezo wa makala hii, leo kiongozi huyo anabainisha namna anavyoumizwa na kushamiri kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia na udhalilishaji visiwani Zanzibar na mbinu ambazo wanajipanga kuzitumia, ikiwamo kuanzisha mahakama maalum ya kushughulikia kesi za makosa hayo.

Rais Mwinyi pia anadokeza kusudio la serikali yake kufanya mabadiliko ya kisheria, ili watuhumiwa wa makosa ya ukatili wa kijinsia na udhalilishaji wasiwe wanapatiwa dhamana kortini. Endelea kupata undani wa mazungumzo ya Nipashe na kiongozi huyo:

SWALI: Kumekuwa na ongezeko la vitendo vya **ukatili wa kijinsia hapa Zanzibar. Serikali yako ina mikakati ipi kudhibiti baa hili?**

**RAIS MWINYI:** Ni kweli, ni eneo moja ambalo kwa sasa ni tatizo kubwa hapa Zanzibar. Suala la udhalilishaji. Takwimu zinaonyesha ni eneo ambalo linazidi kuongezeka.

Ni eneo ambalo serikali lazima tulifanyie kazi kwa nguvu zetu zote. Na ndiyo maana nikaamua kukutana na wadau. Suala hili lina wadau wengi. Tukianza na huku kwenye jamii, kuna suala la la maadili. Kwa kweli maadili yameshuka sana.

Kwa hiyo, tumewaomba wenzetu, viongozi wa dini, tumewaomba wanaharakati, asasi za kiraia mbalimbali kuhakikisha wanatoa elimu ya kurudisha maadili katika jamii.

Tukitoka hapo, makosa yakishafanyika. Je, kwa kiasi gani wamekuwa na ufanisi katika kufuatilia makosa ya udhalilishaji? Kwa sababu ukishindwa kutafuta ushahidi vizuri pale ngazi ya polisi, unakuwa umepoteza ushahidi, unashindwa kuwahukumu wale wanaofanya mambo hayo.

Kwa hiyo, tunalitaka Jeshi la Polisi kufanya kazi ya ziada kuhakikisha linajipanga upya kufanya utafiti, kufanya uchunguzi husika ili hawa watu waende kwenye mkono wa sheria.

Tukitoka hapo, kuna suala la Mkurugenzi wa Mashtaka ambaye ndiye mwenye mamlaka ya kupeleka kesi mahakamani. Naye tumemtaka ofisi yake ijipange vizuri zaidi kuhakikisha wanapeleka kesi nyingi zaidi za hawa watu wanaofanya udhalilishaji, lakini na mahakama yenyewe ishughulikie tatizo la ucheleweshaji wa kesi.

Mahakama inakaa na kesi muda mrefu. Sasa, wengine katika hao wanaodhalilishwa, ni watoto ambao wanashindwa kufika mahakamani kwa muda wote huo na ndani yake kuna unyanyapaa kwenye jambo hili.

Kwa hiyo, tumekubaliana wadau wote kuanzia ngazi ya jamii, polisi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ofisi inayohusika na upimaji wa DNA (vinasaba) na kadhalika, kila mtu ajipange upya ili tuhakikishe kwamba watu wanaofanya makosa haya, basi wanachukuliwa hatua stahiki.




Lakini hatujaishia hapo. Tuna mpango sasa wa kurudi kwenye Baraza la Wawakilishi kufanya sheria ziwe na makucha zaidi. Kwa mfano, tunataka kwenda kuondoa dhamana kwa mtu anayeshtakiwa kwa makosa haya.

Hatua zote hizi zikitekelezwa na wadau wote kama tulivyoazimia, sina shaka kwamba baada ya muda mfupi, tutaona kesi za aina hii zinapungua au kwisha kabisa.

**SWALI: Umelipa uzito mkubwa suala hili kwenye mipango yako. Mpaka sasa kuna watu wanawajibishwa kwa hili?**

**RAIS MWINYI:** Ndiyo. Zipo kesi zinaendelea. Na sasa nimeagiza wote wanaoshughulika na mambo haya, waongeze bidii, kwa maana ya utendaji wa kazi.

Kwa hiyo, zile kesi ambazo bado ziko mahakamani, nimemtaka Jaji Mkuu na timu yake kuhakikisha kwamba tunatengeneza mahakama maalum ili kuondoa ucheleweshaji wa kesi hizi. Ziende haraka na watu wapate haki zao.

Mkurugenzi wa Mashtaka ajipanga vizuri zaidi, polisi wajipange vizuri zaidi. Bado kuna kesi zinaendelea, kuna watu wanahitajika kutoa ushahidi. Wote tunawataka washirikiane vizuri sasa ili kesi hizo zifike mwisho.

**SWALI: Biashara na matumizi ya dawa za kulevya bado tatizo nchini. Serikali yako imejipangaje katika hili?**

**RAIS MWINYI:** Ni kweli, dawa za kulevya ni tatizo lingine. Kama mnavyotambua, Zanzibar inategemea sana uchumi wa utalii. Tuna mpango wa kuimarisha vyombo vyetu vya kupambana na dawa za kulevya.

Pia tuna mpango wa kuhakikisha kwamba maeneo ya kuingilia kama vile bandari na viwanja vya ndege tunaweka ulinzi mkubwa zaidi.

Kwa ujumla, ile taasisi na timu zote zinazopambana na dawa za kulevya, lazima ziimarishwe. Huo ndiyo mpango wa serikali katika hili.

**SWALI: Wakulima wa Zanzibar, hasa wakulima wa mwani na karafuu, watarajie nini kutoka kwa serikali yako?**

**MWINYI:** Nilikutana nao na wakanieleza matatizo yanayowakabili. Wakulima wa mwani wa changamoto kadhaa ikiwamo zana duni. Kwa hiyo, wanatumia muda mwingi, lakini mavuno ni kidogo mno. Wanachangamoto katika kupata masoko, wanashindwa kuuza vizuri na 'wanalaliwa' sana bei wanayopata ni ndogo mno.

Tulichowaahidi ni kwamba tutawasaidia katika kupata zana za kisasa zaidi ili kupata mavuno mengi. Tutawasaidia katika kutafuta wawekezaji wa kuweka viwanda vya kuchakata mwani hapahapa Zanzibar na bei iwe nzuri zaidi na soko la uhakika.

Kwa hiyo, wakulima wa mwani tuliwahakikishia hayo yote kama tunavyofanya kwa wavivu ili nao wafanye kazi zao kwa tija zaidi.

Kwa upande wa wakulima wa karafuu, hili ni zao ambalo kwa Zanzibar ni muhimu sana na serikali iliyopita iliwawekea wakulima bei nzuri sana ya Sh. 14,000 kwa kilo ambayo tunaangalia namna ya kuifanyia kazi, ili tuweze kuchakata karafuu hapahapa Zanzibar.

Tunajua ukiongeza thamani katika karafuu, unaweza ukapata zaidi. Kwa hiyo, tuko katika mazungumzo na waagizaji mbalimbali, waje kuwekeza katika viwanda vya kuchakata karafuu hapahapa ili kuongeza thamani ya zao hilo na wakulima wapate soko zuri na bei nzuri.

Ukishakuwa na viwanda vya kuchakata karafuu hapahapa, utakuwa na uhakika wa soko na bei ya zao hilo itakuwa nzuri, hivyo utoroshaji wa karafuu kwenda nje ya nchi nao utapungua kama si kukoma kabisa, hakutakuwa na haja ya kufanya magendo tena.

Lakini katika kupambana na hili la magendo katika biashara ya karafuu na mazao mengine, serikali imejipanga kuhakikisha ulinzi unaimarishwa. Jeshi kama KMKM linaimarishwa ili kupambana na magendo.

*ITAENDELEA KESHO

HABARI KITAIFA

## Mkandarasi mwendokasi kikaangoni

**Na Elizabeth Zaya**

MKUU wa Wilaya ya Temeke, Gowdin Gondwe, amemtaka mkandarasi wa kampuni inayotengeneza barabara ya mwendokasi ya Mbagala kuhakikisha anafanya kazi hiyo kwa thamani halisi ya fedha anayolipwa.

Gondwe alitoa kauli hiyo jana baada ya kufanya ziara ya kutembelea na kukagua ujenzi unaoendelea katika barabara hiyo.

Alisema baada ya kukagua alibaini kasoro nyingi ikiwamo kuwapo kwa nyufa zilizoanza kujitokeza kwenye barabara hiyo na katika vituo vyake vya kusimama mabasi wakati bado haijaanza kutumika.

"Kwa taarifa nilizonazo ni kwamba ninyi viongozi wa hii kampuni inayotengeneza barabara mnawarubuni vijana wetu waliopo maabara wachakachue matokeo rasmi wanayoyaona kule kuhusu mradi huu na wasipokubaliana na ninyi mnawafukuza kazi," alisema Gondwe.

Kwa upande wake Meneja wa mradi huo, Barakael Mmari, alimhakikishia Gondwe kwamba atafuatilia na kumwandikia kwa maandishi mkandarasi huyo juu ya kinachoendelea katika mradi huo.

## Manyanya ataka kasi miradi ya kimkakati

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Nyasa (CCM), Mhandisi Stella Manyanya, ameishauri serikali kuhakikisha inakamilisha ujenzi wa bwawa la uzalishaji umeme la Mwalimu Nyerere na ujenzi wa reli ya kisasa katika mpango wa tatu wa maendeleo wa miaka mitano ili kuwa mkombozi kwa Watanzania.

Akichangia mpango huo bungeni jana, Mbunge huyo alisema: "Tunapoteza mapato kutokana na usafirishaji mizigo kutoa bandarini kupeleka nchi jirani, wana CCM tuna wajibu wa kuelimisha wananchi ili kujua umuhimu wa miradi hii, tuendelee kuisemea hadi itakapokamilika."

# Wizara yamkana Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Huria

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imewataka wafanyakazi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), kuendelea na kazi na kutoa wito wanafunzi wa chuo hicho kuendelea na masomo kama kawaida.

Kauli hiyo ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetolewa baada ya Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Elifas Bisanda, kutoa waraka wa tahadhari dhidi ya ugonjwa wa corona kwa wafanyakazi na wanafunzi wa chuo hicho.

Februari 8, mwaka huu, ulisambaa waraka wa Prof. Bisanda ukiwatahadharisha wanafunzi na wafanyakazi katika chuo hicho kuchukua tahadhari na pia kuwataka wanafunzi kukaa majumbani na kusoma kwa mtandao.

"Hatutaruhusu wanafunzi na wageni kuingia kwenye kampasi zetu bila sababu maalum, kama kuja kuchukua vyeti au kufanya 'clearance' na pale inapobidi waingie, watakiwe kuvaa barakoa wakati wote.

Waende kule wanakotakiwa kwenda na si kuzurura kila mahali. Utaratibu ufanyike kuwasaidia wanaotaka kutumia maktaba kama ni lazima, wengi wanaitumia maktaba yetu kama mahali pa kujisomea tu," ilisomeka sehemu ya waraka wa Prof. Bisanda.

"Maelekezo haya ni kwa ajili ya makao makuu, vituo vyote vya mikoa na vituo vya uratibu vilivyoko nchini. Nimetoa maoni yangu, kama ushauri, nikiwa nawajibika pia kama kiongozi, kuwalinda wale wote ninaowaongoza."

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Oliva Kato, waraka huo ni batili na maelekezo yaliyotolewa na Prof. Bisanda ni maoni yake binafsi, na hayakuzingatia mwongozo wa udhibiti wa maambukizi ya ugonjwa wa corona.

"Waraka uliotolewa Februari 8, mwaka huu na Prof. Bisanda ni batili, ni maoni yake binafsi, hayakuzingatia mwongozo wa udhibiti wa maambukizi ya ugonjwa wa corona katika shule, vyuo na taasisi za elimu nchini wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wa Mei 27 mwaka 2020," ilieleza taarifa ya Kato.

"Wizara inaelekeza wanafunzi na wafanyakazi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kuendelea na masomo na kazi zao kama kawaida."

"Wizara inatoa rai kwa taasisi zote za elimu nchini kuzingatia maelekezo ya serikali kuhusu udhibiti wa maambukizi ya ugonjwa wa corona. Inatoa onyo kwa viongozi na watumishi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na taasisi zake kuacha kutumia nembo za serikali wanapotoa maoni yao binafsi."



Askari mgambo wakiimarisha ulinzi ili kuhakikisha wafanyabiashara waliohamishwa hawarudi kwenye eneo waliloondolewa ili kupisha upanuzi wa barabara, huko Kibaha Picha ya Ndege, mkoani Pwani jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ajira 12,000 kumwagwa sekta ya afya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa serikali inatarajia kuajiri watumishi wapya 12,476 katika mwaka wa fedha 2020/21, Bunge lilielezwa jana mjini hapa.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mwantumu Zodo.

Mbunge huyo alisema sekta ya afya nchini ina upungufu wa watumishi 16,000 na kuhoji serikali ina mpango gani katika kupunguza tatizo hilo.

"Serikali ina mpango gani katika kukabiliana na changamoto hiyo?" Alihoji.

Dk. Mollel alisema upungufu wa watumishi katika sekta ya afya umetokana na mahitaji mapya yanayotokana na upanuzi wa hospitali za kanda, ujenzi na upanuzi wa hospitali za rufani za mikoa 10.

Alisema pia kukamilika kwa ujenzi wa hospitali za halmashauri 102, kukamilika kwa ujenzi wa vituo vya afya 487, na zahanati 1,198 kumechangia ongezeko la uhaba wa wataalamu wa kada ya afya.

Hata hivyo, alisema serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kukabiliana na uhaba wa watumishi huku akibainisha kuwa katika kipindi cha mwaka 2016 hadi 2020, iliajiri watumishi 14,000.

"Zaidi ya watumishi 565 walipatiwa ajira za mikataba kwa kugharamiwa na makusanyo ya vituo vya kutolea huduma na wengine kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo," alisema.

Pia alisema serikali imeendelea kutoa ajira mbadala ili kujaza nafasi zilizoachwa wazi na watumishi waliostaafu, kuacha kazi au kufariki. "Katika mwaka wa fedha 2020/21, Sekta ya Afya inatarajia kuajiri jumla ya watumishi wapya 12,476,"alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani kupeleka watumishi wengi mkoani Tanga kwa sababu una halmashauri nyingi nchini.

Akijibu swali hilo, Dk. Mollel alisema katika ajira hizo 12,476 watahakikisha maeneo yenye uhitaji maalum wa wahuduma wa afya yatazingatiwa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Wadau waujadili utalii

**MAPEMA** wiki hii, Mbunge wa Arusha Mjini (CCM), Mrisho Gambo, aliiomba serikali kuangalia uwezekano wa kushusha tozo za utalii katika hifadhi za Taifa, zilizotangazwa Julai 2021 kutokana na sekta hiyo kuathiriwa na corona.

Ongezeko la tozo hizo lililenga Hifadhi za Ziwa Manyara, Serengeti, Tarangire na Arusha kwa kipindi cha msimu wa juu wa utalii, huku tozo za sasa zikiachwa kutumika msimu wa chini wa utalii.

Hoja ni kwamba watu wengi wamekosa ajira kama madereva, waongoza watalii pamoja na wafanyakazi wa mahoteli kupunguzwa kazini, kwamba ukanda wa Afrika Mashariki, mfano Kenya kwenye Hifadhi ya Nairobi wamepunguza tozo kutoka Dola za Marekani 43,000 hadi 35,000, Rwanda kutoka Dola 1,500 hadi 500, Uganda kutoka 700 hadi 500. Aliiomba serikali kuangalia athari za corona kwenye masuala ya ajira na mengine, lakini Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, alisema wakati tozo za serikali zikiwa chini kampuni za utalii zimekuwa zikitoza wageni fedha nyingi, huku kukiwa na usiri ambao unainyima serikali fedha.

Kwamba hakuna uthibitisho wa takwimu za wageni wengi kufuta safari zao kuja nchini kutokana na ongezeko la tozo, huku Waziri wa wizara hiyo, Dk. Damas Ndumbaro, akisema licha ya nchi za Afrika Mashariki kupunguza tozo ya utalii, Tanzania viwango vyake bado vipo chini.

Licha ya serikali kukinzana na Gambo, lakini tunaona yanahitajika mazungumzo ya wadau wa sekta ya utalii kutokana na ukweli kuwa athari za corona ni kubwa na zinaumiza wengi duniani. Kwa kuwa kadri maambukizi yanavyozidi katika nchi zenye idadi kubwa ya watalii wanaokuja nchini.

Ni muhimu pande zote zikajadiliana kwa kuwa hali ilivyo wadau wa utalii wanahitaji kuendelea kuwapo kutoa ajira na kulipa kodi za serikali.

Katika kipindi kigumu cha athari za ugonjwa huu ndiyo wakati wa kuzungumza kuifanya sekta izidi kustawi. Tunatambua umuhimu wa sekta katika kuchangia kwenye pato la taifa na kutoa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja.

Mchango wa sekta ya utalii kwa maendeleo ya watu na taifa ni mkubwa, mathalani katika maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Jamii (WMA), walipata kipato kutokana na shughuli za utalii.

Fedha hizo ziligawanywa kwenye vijijini vilivyotoa maeneo yakawa WMA, na walizitumia kwa kadri ya vipaumbele vyao kama kujenga zahanati, vituo vya afya, huduma za maji, barabara na nyinginezo ambazo moja kwa moja ziligusa maisha ya wananchi na waliachana na michango.

Sasa fedha hizo hakuna na kwa sasa hata wawekezaji waliopo kwenye maeneo yao atashindwa kulipa kodi, jambo ambalo litawarudisha katika kuchangishana ili kukamilisha malengo aliyojiwekea katika sekta husika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Halfan Chuzi

## Hongera mradi wa makazi mapya Magomeni Kota kwa 'Hapa Kazi'

**HONGERA** TBA, nikimaanisha Wakala wa Majengo Tanzania, kwa kuonyesha juhudi za dhati tangu walipothaminiwa na Rais Dk. John Magufuli, kuhakikisha wakazi wa Magomeni Kota, jijini Dar es Salaam waliobomolewa nyumba zao, wanapata makazi salama na stahiki.

Licha ya kuwapo ramani elekezi kutoka serikalini, lakini TBA imeonyesha ubunifu mkubwa katika kuandaa majengo hayo. Ni jambo linalostahili pongezi na wakati huo huo, wanakuwa mfano wa kuigwa.

Meneja Mradi wa TBA, Bernard Mayemba, anaeleza kuwa wanaorodhesha ubunifu wa ziada walioongeza katika mradi ukubwa wa vyumba, uzio unaozunguka nyumba na kibanda cha mlinzi mlangoni makazi hayo, ikiwa ni namna ya kuwahakikisha usalama wa kila anayeingia na kutoka mahali hapo.

Pia ni aina ya ramani itakayozungukwa na fremu za maduka, ili wakazi hao tarajiwa kutoka ndani wapate urahisi wa kupata mahitaji.

Ni mradi unaotarajiwa kutengeneza makazi ya zaidi ya kaya 600, jambo linalozaa ulazima wa kuwa na sehemu ya upatikanaji huduma hizo muhimu za kijamii.

Kwa mujibu wa ufafanuzi wa kiufundi uliopo, mradi huo wa makazi Magomeni Kota, kwa sasa umefikia asilimia 90 kukiwapo matarajio makubwa ya kukabidhiwa kwa wahitaji ndani ya muda mfupi ujao.

Ndani ya mwendelezo wa mradi huo wa makazi, ambayo awali kulikuwapo nyumba kongwe kihistoria, hata kabla ya uhuru nchini, Mkuu wa Wilaya Kinondoni, Daniel Chongolo, alifanya ziara mahali hapo kutembelea mradi huo na alionyesha kuridhishwa na kasi ya uendelezaji wake.

Mkuu huyo wa Wilaya, Chongolo, pia alikuwa na mambo kadhaa ya ushauri, alipotamka: "Kipindi cha nyuma kidogo nilikuja hapa nikakuta mradi huu una asilimia 60, lakini leo ni tofauti kabisa na nilivyokuja mwanzo. Lakini sasa, naambiwa mradi umefikia asilimia 90. Kwa hiyo, sina budi kuwapongeza TBA.

"Sisi kama viongozi tutaendelea kusimamia kwa umakini miradi ambayo imeanzishwa na Rais Magufuli, ili kuhakikisha kila mwananchi anapata stahiki yake," anasema.

Pia Chongolo aliiomba TBA kuweka utaratibu utakaomchukulia hatua yeyote atakayeharibu miundombinu husika, pindi watakapohamia na kubainika kuwapo chochote chenye kuashiria

kuharibika miundombinu, iliyowekwa kwa mfumo wa kisasa kisasa zaidi.

"Kuna lifti, njia za umeme, pamoja na vitu vingi ambavyo vinahitaji umakini mkubwa kwa wakazi. Wekeni utaratibu wa kutoa elimu kwa kila nyumba, namna yakuweza kutumia vitu vilivyomo humo ambavyo kwa kiasi kikubwa vinaambatana na mifumo ya kisasa zaidi," anasema.

Pia kuna ushuhuda mwingine kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elius Mwakalinga, alipofanya ziara ya kushtukiza mahali hapo.

Ni aina ya ushuhuda ulioko katika mtazamo uleule kama wa Mkuu wa Wilaya, Chongolo, alipoonyesha kuridhishwa na namna TBA, walivyochapa kazi ndani ya mradi huo tajwa.

Anasema, katika ziara yake ya ukaguzi ikizingatiwa kilichokuwa kikifanyika kilikuwamo ndani ya taaluma yake Oktoba mwaka jana katika kipindi alichozuru Chongolo, alikuta mradi umefikia asilimia 81 ya utekelezaji.

Pia ni muda mfupi baadaye aliporudi Mwakalinga alikuta katika kiwango cha asilimia 90, hapo hakusita kuimwagia sifa RBA kwa kasi bora ya uchapaji kazi.

Vilevile, aliipongeza TBA kwa kuzingatia maelekezo aliyoyatoa katika ziara ya mwanzo na kuonyesha ubunifu kwa ujenzi wa majengo ya kupokelea wageni na majengo ya maduka yatakayotoa huduma kwa wakazi hao wa Magomeni Kota.

Ni ziara iliyokutana pia na agizo la Mwakalinga, kupitia Idara ya Miliki kumweka ofisa maalum wa kupokea maombi mbalimbali, wakiwamo wateja wanaopenda ama kuuziwa au kupangisha nyumba hizo.

Kwa mujibu wa Mwakalinga, ni jambo litakalosaidia kutambua mahitaji ya soko la nyumba nyingine zitakazojengwa mkabala na mradi unaoendelea kujengwa.

**HABARI KITAIFA**

# Balozi Marekani, Katibu Mkuu EAC wateta

**Na Asraji Mvungi,** ARUSHA

BALOZI wa Marekani nchini, Donald Wright, amekutana na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Balozi Liberate Mfumukeko, jijini hapa na kueleza kuwa utawala mpya wa Marekani unatarajia kuendeleza ushirikiano wa jumuiya hiyo.

Aidha, Balozi Wright amewasilisha hati ya utambulisho kwa katibu mkuu huyo wa EAC.

Akizungumza baada ya kikao chao cha ndani, Balozi Wright alitaja baadhi ya sekta zinazotarajiwa kuendelea kupata misaada kutoka Marekani kuwa ni kilimo, afya, nishati, mazingira, kukuza demokrasia na pia uwezeshaji wa vijana.

Kwa mujibu wa Balozi Wright, lengo ni kuendelea kuona EAC yenye umuhimu mkubwa, inaendelea kukua sambamba na jumuiya zingine za kikanda.

"Marekani imejitolea kusaidia nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ili ziendelee kukuza uchumi na pia utulivu wa kisiasa na pia imejitolea kushirikiana na jumuiya zingine za kikanda na kimataifa sambamba na Umoja wa Mataifa na AU (Umoja wa Afrika,"alisema Balozi Wright.

Naye Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo, Balozi Mfumukeko, alisema hatua hiyo ni mwendelezo wa ushirikiano mzuri unaoendelea kati ya Marekani na nchi za EAC.

"Kwa muda mrefu sasa nchi za EAC zimekuwa zikinufaika na misaada kutoka Marekani ambayo imekuwa ikisaidia sekta mbalimbali katika nchi wanachama. Katika mazunugumzo yetu pia nimemweleza baadhi ya maeneo muhimu yanayohitaji kupewa kipaumbele kwenye uwezeshaji hasa sekta ya afya na pia uwekezaji," alisema Balozi Liberate Mfumukeko.

Pia Balozi Mfumukeko alimweleza Balozi Wright hatua iliyofikiwa katika utekelezaj wa mchakato wa kuondoa vikwazo vya kibiashara kwenye forodha za nchi wanachama na itifaki za soko la pamoja na pia kuelekea kwenye sarafu moja mchakato ambao unatarajiwa kukamilika ifikapo mwaka 2024.

Katika hatua nyingine, Balozi wa Pakistan nchini, Muhammad Saleem, alitembelea na kukabidhi hati ya utambulisho kwa katibu mkuu wa EAC na pia walifanya mazungumzo yanayolenga kuongeza fursa za ushirikiano kati ya Pakistan na nchi za EAC.

Pia wamekubaliana kuwawezesha wadau wa sekta za kiuchumi, wakiwamo wafanyabiashara kujenga mtandao utakaowawezesha wananchi wa nchi hizo kushirikiana.

Akizungumzia na mgeni wake huyo, Balozi Mfumukeko alisema Pakistan ni miongoni mwa nchi zinazoshirikiana kwa karibu na nchi wanachama wa EAC mashariki katika sekta mbali mbali za kiuchumi, biashara na huduma.



Balozi wa Marekani hapa nchini, Donald Wright (kushoto), akisalimiana na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Balozi Liberate Mfumukeko, kwa staili, wakati akikabidhi hati ya utambulisho, makao makuu ya jumuiya hiyo, jijini Arusha jana. **PICHA: ASRAJI MVUNGI**

# DED ataka kasi ya ukusanyaji mapato

**Na Stevie Chindiye,** NAMTUMBO

HALMASHAURI ya Wilaya Namtumbo mkoani Ruvuma, imewataka watendaji wa vijiji na kata kukusanya mapato kupitia vitambulisho vya ujasiriamali na yale yatokanayo na kodi za majengo na mabango.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Evance Nachimbinya, alitoa maagizo hayo, jana, alipokuwa akizungumza na watendaji wa kata na vijiji katika ukumbi wa halmashauri mjini hapa.

Alisema kodi ya majengo na mabango ilikuwa inakusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) lakini kwa sasa serikali imerudisha serikali za mitaa ili kurahisisha ukusanyaji huo.

Kutokana na hali hiyo, Nachimbinya aliwaagiza watendaji hao kuwa kabla ya kuanza ukusanyaji, wanatakiwa kuwasilisha taarifa za majengo yanayostahili kulipiwa kodi na idadi ya mabango yaliyoko katika vijiji vyao ofisini kwa mkurugenzi.

Ofisa Biashara wa Halmashauri, Revocatus Kavishe, aliwaambia watendaji hao kuwa wanatakiwa kufuata sheria, taratibu na kanuni katika kusajili walipa kodi za majengo na si kupokea maelezo yanayolenga kukwepa kulipa kodi na kimsingi hayapo katika sheria.

Kavishe alisema uzoefu unaonyesha kuwa wako watendaji katika kutekeleza majukumu yao , hawasimamiii kanuni na sheria na badala yake husikiliza maelezo ya watu wenye nia ya kukwepa.

Alisema uzoefu alioupata katika ukusanyaji wa fedha za vitambulisho vya wajasiriamali umempa mwanga kwamba wako watendaji ambao hawakuuza vitambulisho kwa baadhi ya wafanyabishara wadogo badala ya kufuata sheria na kanuni zilizopo za wajasiriamali wote wanahitajika kuwa na vitambulisho badala ya kupokea maelezo.

Mtendaji wa mamlaka ya mji mdogo wa Namtumbo, Mario Mwageni, alisema kwa jambo hilo si geni lakini alihoji sheria ya ukusanyaji inasemaje katika maeneo mengine ambayo si mamlaka ya mji mdogo kwa kuwa ukusanyaji katika sheria inayotumika inaishia kukusanya kodi ya majengo katika mamlaka ya miji midogo pekee.

# TBS yaweka msimamo ukaguzi magari

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limesema hakutakuwa na kurudi nyuma katika kutekeleza agizo la serikali la ukaguzi wa magari kufanyika nchini badala ya nje ya nchi kama ilivyokuwa awali.

Kauli hiyo ilitolewa jijini Dar es Salaam jana na Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Yusuf Ngenya, wakati akifungua mkutano wa mawakala wa forodha, waagizaji magari nje ya nchi na wauzaji wa magari kwa lengo la kuwawezesha kuwa na uelewa mzuri wa utekelezaji wa mpango huo.

Alisema TBS imekuwa ikiendesha shughuli zake kwa viwango na kwamba moja kati ya takwa la viwango ni kukaa na wadau ili kupata mwafaka wa lile ambalo wanataka kulifanya ili lifanyike bila vipingamizi na kwa ufanisi.

"Ndiyo maana tumewaita hapa ili tuwe na uelewa wa aina moja kwa lengo la kuhakikisha mpango huu unatekelezwa bila malalamiko yoyote. Tunafikia hatua hiyo kwa kukaa pamoja na kuweza kuona changamoto zinazoweza kujitokeza na kupata majibu yake ili utekelezaji utakapoanza majibu yote tuwe nayo," alisema Dk. Ngenya.

Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora wa TBS, Lazaro Msasalaga, alisema uamuzi huo wa serikali haukutoka hewani, bali ni kutokana na maoni mbalimbali ya wadau.

Miongoni mwa maoni hayo kwa mujibu wa Msasalaga ni kutaka ukaguzi huo ufanyike nchini, kwani nje ya nchi wamekuwa wakipata usumbufu na kuingia gharama kubwa.

"Pia walishauri zile fedha ambazo wamekuwa wakilipa nje ya nchi kwa ajili ya ukaguzi wa magari zilipwe hapa nchini ili zisaidie kujenga uchumi na kuongeza ajira kwa nchi yetu," alisema Msasalaga.

Alifafanua kuwa tayari Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imetenga yadi tatu ambazo zitatumika kwa ajili ya ukaguzi huo akiitaja ya kwanza kuwa ni ya Ro-Ro ambayo itakuwa na seti nane za vifaa kwa ajili ya ukaguzi wa magari madogo.

Yadi ya pili, kwa mujibu wa Msasalaga, ni ya Copper ambayo itakuwa na seti moja ya vifaa kwa ajili ya ukaguzi wa magari makubwa na yadi ya tatu itakuwa ni ya Lighter quay ambayo nayo itakuwa na seti moja kwa ajili ya ukaguzi wa magari makubwa.

## Waonywa kulima njia wanyamapori

**Na Stevie Chindiye,**

TUNDURU

SERIKALI imewataka wananchi kuacha kufanya shughuli za kilimo kwenye maeneo ya mapitio ya tembo ili kujikinga na matukio ya kuuawa na wanyama hao.

Tahadhari hiyo ilitolewa juzi na Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Fatuma Kizigo, wakati akizungumza na wadau wa uhifadhi wa wanyamapori katika kikao kilichofanyika katika Kijiji cha Milonde, Kata ya Matemanga wilayani hapa.

Kizigo ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, alisema iwapo wananchi watazingatia hayo pamoja na mafunzo hayo yakitumiwa vizuri, yanaweza kuleta suluhisho la kudumu la mauaji yanayosababishwa na tembo.

Naye mdau wa uhifadhi, Rashid Chimwaya, alisema ongezeko la wanyama katika maeneo ya hifadhi limesababisha matukio mengi ya uhalibifu wa mazao ya wakulima pamoja na mauaji ya wananchi katika maeneo mbalimbali ya wilaya ya Tunduru.

Alisema matukio mengi ya wananchi kuuawa yamekuwa yakitokea wakati wakiwafukuza kwa kutumia mbinu za kupiga madebe, kuwasha moto na kuwamulika na tochi ili kunusuru mazao yao kushambuliwa na kusababisha kukumbwa na njaa.

Takwimu kutoka ofisi ya wanyamapori Wilaya ya Tunduru zinaonyesha kuwa wananchi 24 walifariki dunia na wengine 20 walijeruhiwa na kupata umemavu wa maisha katika matukio yaliyosababishwa na wanyamapori.

Ofisa Wanyamapori wa Wilaya ya Tunduru, Limbega Ally, alisema matukio hayo yalitokea kuanzia mwaka 2015 hadi 2020.

# RC Kunenge awawashia moto watendaji

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Aboubakar Kunenge, amewataka viongozi ngazi za mitaa kuhakikisha wanashughulikia ipasavyo kero na changamoto mbalimbali kwenye mitaa yao.

Pia amewataka kuhakikisha wanatoa taarifa mapema pale wanapobaini kuna jambo ambalo liko juu ya uwezo wao ili lishughulikiwe na ngazi za juu.

Kunenge alisema hayo jana wakati wa kikao chake na watendaji na wenyeviti wa mitaa jijini Dar es Salaam, huku akisisitiza kuwa ni jambo la fedheha kuona kiongozi wa ngazi ya juu anashughulikia kero ya mtaa wakati wahusika wa ngazi ya mtaa wapo na wanafanya mambo yao tu.

Pia Kunenge aliwaelekeza watendaji wa mkoa kuhakikisha wanasimamia ipasavyo ukusanyaji wa mapato ikiwa ni pamoja na kubuni vyanzo vipya, kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

Alisisitiza kuwa ukusanyaji wa mapato usiwe wa kero wala wa kuua biashara za watu huku akiwataka viongozi wa mitaa kusimamia ipasavyo usafi wa mazingira kwenye mitaa yao ili kuwakinga wananchi na magonjwa ya mlipuko.

Sambamba na hilo, aliwasisitiza viongozi hao kutoa taarifa pindi wanapobaini uwapo wa watu wanaohatarisha usalama ikiwamo kufichua nyumba zinazogeuzwa madanguro, wanaowahifadhi wahamiaji haramu, wanaowatumia wenye ulemavu kujinufaisha na wauzaji wa dawa za kulevya.

Kadhalika alizielekeza taasisi za umma zilizoko ndani ya jiji kuhakikisha zinashirikiana na watendaji wa mitaa kwa kuwa hao ndio wako karibu na wananchi na ndio wanaozijua zaidi kero za mtaa.



Mkurugenzi wa M-Pesa, Epimack Mbeteni (katikati), akishuhudia mteja wa Vodacom, Aziza Iwvata (kushoto), akilipa kwa kutumia huduma ya "M-pesa Lipa kwa Simu" kwenye duka la Red Tag, jijini Dar es Salaam jana, ambapo wateja wa Vodacom watapata punguzo la asilimia 10 katika msimu huu wa wapendanao. Kampuni hiyo, inatekeleza mkakati wa kuhakikisha jamii inaondokana na matumizi ya pesa taslimu. Kulia ni mtoa huduma wa duka hilo, Asayo Hirashi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbunge ataka kufutwa kodi vifungashio korosho

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MBUNGE wa Nanyamba (CCM), Abdalah Chikota, ameitaka serikali kufuta kodi na tozo katika vifungashio vya zao la korosho ili kupunguza gharama za uzalishaji na kuvutia wawekezaji wa kigeni na wazawa.

Chikota alikuwa akichangia jana mjadala wa mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya mpango, bajeti ya serikali na mpango wa maendeleo wa taifa kwa mwaka 2021/22 na mapendekezo ya mpango wa tatu wa maendeleo wa taifa wa miaka mitano wa mwaka 2021/22 -2025/26.

"Nashauri tukose fedha kidogo leo ili tupate fedha nyingi baadaye. Hii inawezekana tuondoe tozo na kodi zilizopo wakati wa uungizaji wa mashine za kubangua korosho ili mashine nyingi ziingizwe.

"Vilevile nashauri tuweke vivutio maalum kwa wawekezaji wapya, na tatu tuondoe kodi na tozo katika vifungashio, faida yake ni kwamba tutapunguza gharama, hivyo tutapata wawekezaji wengi," alisema.

Mbunge huyo alisema kuwa ubanguaji wa kisasa ndiyo njia pekee ya kuhakikisha korosho ya Tanzania inapata bei nzuri kwenye soko la dunia.

"Lengo la kuweka 'export levy' (tozo za mauzo ya nje ya nchi) ni ili wasafirishe korosho ghafi. Uwezo wetu wa kubangua korosho katika viwanda vyetu ni tani 70,000 na sasa hivi tunazalisha kama tani 120,000 na korosho nyingi tunaiuza ikiwa ghafi," alisema Chikota.

Kwa mujibu wa Chikota, kiwanda kidogo cha ubanguaji mtaji wake ni Sh. milioni 60 na kwa sababu korosho inazalishwa katika zaidi ya mikoa 12, ni vyema serikali ikaelekeza fedha za mfuko wa vijana, kuanzisha viwanda vidogo vya kubangua korosho ili kuongeza ajira.

Naye Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Halima Mdee, aliitaka serikali kuja na mpango mahususi wa kuhakikisha sekta binafsi inashamiri kwa kuwa hivi sasa ushiriki wao katika ujenzi wa taifa una matatizo.

Mdee akichangia mjadala huo alisema: "Tufanye tathmini kuona tumekosea wapi tunapoingia mpango wa tatu. Kwenye kilimo, serikali itengeneze miundombinu wezeshi maana tuna mifumo thabiti ya umwagiliaji.

"Nashauri kupanga ni kuchagua hivyo tuangalie sekta zinazogusa wananchi wengi ikiwamo ya kilimo maana inachangia pato la taifa kwa asilimia 26," alisisitiza.

HABARI KITAIFA

# TIB yapiga jeki wilaya viti na meza shuleni

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Maendeleo (TIB), imeunga mkono juhudi za serikali za kuhakikisha mazingira ya kujifunzia yanakuwa bora kwa kuchangia viti 100 na meza 100 kwa ajili ya shule za Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi mkoani Kagera.

Akizungumza baada ya kukabidhi msaada huo, Meneja wa Kanda ya Ziwa benki hiyo, Emmanuel Bushiri, alisema benki inatambua kuwa elimu ni moja ya sekta muhimu kwa maendeleo ya nchi.

Alisema mchango walioutoa kwa Halmashauri hiyo umelenga kuhakikisha wanafikia malengo ya kuongeza uandikishaji wa wanafunzi.

Naye, Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti aliishukuru benki hiyo kwa msaada huo uliolenga kuongeza idadi uandikishaji wa wanafunzi na kutoa elimu bora ili kuharakisha maendeleo ya mkoa huo.

# Manyanyaso ya kingono kwa waandishi Dar tatizo

**Na Salome Kitomari**

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), kimesema asilimia 52 ya waandishi wa habari walihojiwa kuhusu rushwa ya ngono, hawakuwa tayari kueleza manyanyaso wanayokutana nayo.

Akizungumza wakati wa kupokea matokea ya utafiti wa hali ya rushwa ya ngono kwenye vyombo vya habari, Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Rose Reuben, alisema asilimia 48 walijieleza juu ya manyanyaso wanayopitia.

Alisema utafiti huo ulifanyika kwa wachache wa jijini Dar es Salaam anaofanyakazi katika vyombo vya magazeti, radio na televisheni, kwa lengo la kuangalia hali ilivyo ndani ya vyombo vya habari na kama kuna mifumo ya kuripoti taarifa hizo.

Kwa mujibu wa Reuben, utafiti huo ulihusisha wahariri waandamizi, waandishi wa habari waandamizi, waajiri, asasi zisizo za kiserikali, vyuo vya uandishi wa habari, waandishi wa habari wa kujitegemea, wenye mikataba midogo na waliopo mafunzoni wanaokwenda kwenye vyombo hivyo kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo.

"Utafiti ulibaini kuwa rushwa haipo kwa wanawake pekee bali hata wanaume, wengi hawasemi kutokana na desturi ya kunyamaza. Tulitaka kujua ukubwa wa tatizo kwa waandishi wa habari ndani ya vyombo vya habari," alisema.

> **"Utafiti ulibaini kuwa rushwa haipo kwa wanawake pekee bali hata wanaume, wengi hawasemi kutokana na desturi ya kunyamaza. Tulitaka kujua ukubwa wa tatizo kwa waandishi wa habari ndani ya vyombo vya habari," alisema.**

Akiwasilisha matokeo ya utafiti kwa niaba ya mtafiti, Meneja Ufuatiliaji na Tathmini wa TAMWA, John Ambros, alisema ilibainika vyanzo vya rushwa ya ngono ndani ya sekta ya habari ni ujira mdogo huku baadhi ya wanahabari wanawake na wanafunzi walio kwenye mafunzo kwa vitendo kushawishi mabosi zao ili kupata upendeleo.

"Baadhi ya wanawake hawana uwezo wa kazi wanatumia ushawishi wa ngono kwa mabosi zao ili kulinda ajira zao," ilisema sehemu ya utafiti huo."

Aidha, TAMWA ilishauri kuwapo kwa sera ya jinsia ndani ya vyombo vya habaro ambayo vyombo vingi vya habari havina pamoja na mifumo ya kutoa taarifa kwa matukio kama hayo.

Naye, Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Dar es Salaam, Irene Mark, alisema licha ya kuwa na utaratibu maalum kwa waandishi wa habari kuripoti taarifa za manyanyaso ya kingono wanayofanyiwa na viongozi zao, lakini hawatumii nafasi hiyo kutoa taarifa hizo, na kuwashauri waandishi kutoa taarifa hizo ili kusaidia kupunguza au kukomesha vitendo hivyo.



Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brig. Jen. Marco Gaguti (kushoto), akizungumza baada ya kukabidhiwa seti 100 za viti na meza na Meneja wa Kanda ya Ziwa wa Benki ya Maendeleo TIB, Emmanuel Bushiri (kulia), kwa ajili ya kuchangia uboreshaji wa utoaji wa elimu ya sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi, mkoani humo juzi. Katikati ni Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Projestus Tegamaisho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC aja na dawa ya migogoro ya ardhi

**Na Gurian Adolf, NKASI**

WILAYA ya Nkasi mkoani Rukwa, imevitaka vijiji kupitia halmashauri kuanza kufikiria namna bora ya kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi, ili kumaliza migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

Mkuu wa wilaya hiyo, Said Mtanda, aliyasema hayo wakati akizindua mradi wa utetezi wa upatikanaji wa ardhi bora kwa wazalishaji wadogo ili kuwa na uhakika wa chakula ambao unatekelezwa na shirika lisilo la kiserikali la MIICO.

Alisema iwapo vijiji vyote wilayani humo vitakuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi, kila kundi litaheshimu lingine, kwa maana wafugaji hawatachungia mifugo yao upande wa wakulima wanafanya shughuli zao za kilimo.

Alisema umefika wakati kwa halmashauri ya Nkasi kuwa na mpango huo, na iwapo hilo litafanimiwa, wakulima watazalisha mazao ya chakula bila migogoro na hivyo kuongeza upatikanaji wa chakula na pia kuondoa changamoto zinazotokana na uhaba wa chakula.

# FCS kutumia bil. 10/- kutoa elimu

**Na Onesmo Andrea, SJMC**

ASASI ya Foundation for Civil Society (FCS) imekusudia kutumia Sh. bilioni 10 kwa ajili ya kuziwezesha asasi za kiraia kutoa elimu kwa jamii kwa masuala mbalimbali.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Meneja miradi wa FCS, Francis Uhadi, wakati wa mkutano wa asasi na wadau kwa lengo la kufanya tathmini ya utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka uliopita na kuweke mikakati ya kipindi kipya.

Alisema malengo ya asasi ni kuhakikisha wananchi wanawezeshwa kielimu kupitia miradi hiyo, ili kutoa mabadiliko chanya kwa jamii

Alisema tangu kuanzishwa kwa utaratibu wa ufadhili wa miradi hiyo miaka minne iliyopita, asasi hiyo kwa kutumia wadau wake imefanikiwa kutoa elimu kwa jamii kubwa kupitia asasi zaidi ya 150 zinazofanya kazi na taasisi hiyo.

"Asasi yetu imekuwa ikifanya kazi na wadau tofauti, tofauti kutoka mikoa yote ya Tanzania bara na visiwani, lengo ni kuhakikisha elimu inawafikia wananchi wote na kutatua changamoto zinazojitokeza," alisema Uhadi.

Naye, Mkuu wa idara ya tathimini, ufuatiliaji, tafiti na mafunzo wa FCS, Gestadi Haule alisema katika kipindi cha mwaka jana asasi hiyo imetekeleza majukumu yake kikamilifu licha ya changamoto ya ugonjwa wa COVID-19.

# Utoaji mikopo halmashauri waongezeka

TANGU kuanza kutumika kwa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 mwaka wa fedha 2018/19 na 2019/20, halmashauri 79 zimetoa mikopo kwa asilimia 100 huku 54 zimetekeleza kwa asilimia zaidi ya 85, imeelezwa.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dk. Festo Dugange, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Asia Halamga.

Mbunge huyo alihoji Halmashauri ngapi nchini zimetekeleza kwa asilimia 100 Sheria ya Utoaji Mikopo asilimia 10 ya makusanyo ya ndani kwa makundi ya vijana, kinamama na watu wenye mahitaji maalum.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema utekelezaji huyo umeongeza mikopo inayotolewa na halmashauri nchini ikilinganishwa na kipindi kabla ya kufanya marekebisho ya sheria.

Alisema katika mwaka wa fedha 2017/18 (kabla ya marekebisho ya sheria) Sh. bilioni 26.1 zilitolewa mwaka wa fedha 2018/19 na baada ya marekebisho ya sheria, Sh. bilioni 42.06 zilitolewa na mwaka wa fedha 2019/20 mikopo iliyotolewa ilikuwa Sh. bilioni 40.7.

Dk. Dugange alisema kwa mujibu wa Kifungu namba 24 (2) cha Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za mwaka 2019, mkurugenzi yeyote ambaye atashindwa kusimamia utekelezaji wa kanuni hizo atakuwa ametenda kosa la kinidhamu na mamlaka yake ya nidhamu inaweza, kwa kadri itakavyoona inafaa, kumchukulia hatua za kinidhamu.

Pia alisema takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa hali ya utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake vijana na watu wenye ulemavu katika halmashauri nchini imeimarika hasa baada ya kufanya marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 yaliyofanyika Julai, 2018.



Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Elias Kwandikwa akijibu maswali kwenye kikao cha saba, mkutano wa Pili wa Bunge la 12, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kata 1,400 hazina mawasiliano ya simu

BUNGE limeelezwa kuwa kata 1,365 kati ya 3,956 Tanzania Bara bado hazijafikiwa na huduma ya mawasiliano.

Aidha, serikali inatarajia mwezi huu kutangaza zabuni ya awamu ya sita ya kufikisha huduma za mawasiliano katika kata 74 zenye vijiji 206.

Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Andrea Kundo, alisema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mbulu Vijijini (CCM), Flatey Massay.

Mbunge huyo alitaka kujua ni lini minara ya simu itejengwa katika kata za Endahagichen - Ndamilay, Mewadan - Magong na Endaghadat - Qamtananat ambazo hazina mawasiliano ya simu.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri alisema kata hizo bado hazina mawasiliano zikiwemo kata za Jimbo la Mbulu Vijijini na wadi 16 kati ya wadi 111 zilizoko Zanzibar. Aidha, alisema serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) inavifanyia tathmini vijiji vya kata za Endahagichen - Ndamilay, Mewadan - Magong na Endaghadat - Qamtananat na hatimaye vitaingizwa katika orodha ya vijiji vitakavyojumuishwa katika zabuni zinazotarajiwa kutangazwa katika mwaka wa fedha wa 2020/21.

Kundo alisema serikali kupitia mfuko huo pamoja na wadau wengine wa sekta ya mawasiliano ina jukumu la kufikisha huduma za mawasiliano katika maeneo yote ya vijijini na mijini yasiyo na mvuto wa kibiashara.

Alibainisha mpaka sasa jumla ya kata 633 zimepata huduma za mawasiliano nchi nzima ambapo ujenzi unaendelea katika kata zingine 361 kupitia ruzuku ya Serikali.

"Watoa huduma kwa uwekezaji wao wamefikisha huduma za mawasiliano katika kata 1692,Januari 25, 2021 tulisaini (tulitia saini) mikataba ya kufikisha huduma za mawasiliano katika kata 59 zenye vijiji 166 katika zabuni ya awamu ya tano,"alisema.

Aliongeza kuwa serikali kupitia UCSAF ina miradi 15 katika jimbo la Mbulu Vijijini katika kata 13 na kata zenye miradi ya kufikisha huduma za mawasiliano ni pamoja na Yaeda Ampa, Yaeda Chini, Maghang, Masieda, Bashay, Eshkesh, Geterer, Gidihim, Hayderer, Maretadu, Masqaroda, Endamilay, na Tumati.

Kundo alisema minara 14 imekamilika kujengwa katika kata 12 kati ya minara 15 inayopaswa kujengwa, hii ni sawa na asilimia 87.5 ya miradi yote katika jimbo hilo. Aliongeza ujenzi wa Mnara uliopo katika Kata ya Endamilay haujakamilika ambapo Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) limepanga kukamilisha ujenzi wa mnara huo kabla ya mwisho wa Juni, mwaka huu.

Alisisitiza kuwa serikali kupitia UCSAF inavifanyia tathmini vijiji vya kata za Endahagichen - Ndamilay, Mewadan - Magong na Endaghadat - Qamtananat na hatimaye vijiji husika vitaingizwa katika orodha ya vijiji vitakavyojumuishwa katika zabuni zinazotarajiwa kutangazwa katika mwaka huu wa fedha yaani 2020/2021.

## Mbunge ataka ruksa wanunuzi binafsi kokoa

MBUNGE wa Viti Maalum (CHADEMA), Sophia Mwakagenda, ameitaka serikali kuruhusu kampuni binafsi kuendelea kununua kokoa.

Akiuliza swali bungeni jana, mbunge huyo alisema serikali ilizuia kampuni binafsi kununua kakaa katika wilaya za Kyela na Rungwe na serikali na vyama vya ushirika havina uwezo wa kununua kokoa hizo kwa wakulima.

"Je ni lini serikali itaruhusu tena kampuni binafsi kuendelea kununua kokoa?,"alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema serikali haijazuia kampuni binafsi kununua kokoa kwa wakulima bali imezuia mfumo wa ununuzi wa ulanguzi maarufu kama 'njemke' ambao umekua ukimnyonya mkulima.

Alisema serikali kupitia mfumo wa vyama vya ushirika imekua ikikusanya na kuuza mazao hayo kupitia minada ya wazi katika kusaidia kutambua bei za mazao hayo.

"Kwa kutumia utaratibu wa ushirika wakulima waliuza kokoa kwa mfumo wa stakabadhi ghalani na bei ya kokoa ilipanda kutoka sh. 3,000 hadi 4,500 kwa kilo mwaka 2016/17 hadi kufikia Sh. 5,000 kwa kilo mwaka 2019/20," alisema Bashe.'

Alibainisha kuwa katika mfumo huo wakulima hupeleka kokoa katika vyama vya msingi na kupewa asilimia 60 ya bei ya soko ya Sh. 4,200.

"Baada ya mnada kufanyika wakulima hupewa kiasi cha fedha kilichobaki ili kufikia bei ya mnada kwa kuzingatia gharama za usafiri, uhifadhi, ushirika na ushuru," alisema.

Aidha, alisema bei hiyo iko juu ukilinganisha na bei ya wanunuzi binafsi kabla ya ushirika na kutokana na faida iliyopatikana kupitia kuuza mazao katika ushirika, Serikali haitaruhusu kampuni binafsi kununua kokoa kwa wakulima kwa kununua bei ndogo ambayo haitakuwa na uwiano wa bei sawa baina ya wakulima.

Aidha, alisema serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika itaendelea kuimarisha na kujenga uwezo wa vyama vya msingi vya ushirika ili kununua kokoa yote kwa wakulima na kuwasaidia wakulima kupata pembejeo sambamba na kuwa na nguvu ya pamoja katika kusimamia bei ya mazao ya wakulima.

**"Kwa kutumia utaratibu wa ushirika wakulima waliuza kokoa kwa mfumo wa stakabadhi ghalani na bei ya kokoa ilipanda kutoka sh. 3,000 hadi 4,500 kwa kilo mwaka 2016/17 hadi kufikia Sh. 5,000 kwa kilo mwaka 2019/20," alisema Bashe.**



Ukurasa 12

**Jitihada za 'Operesheni Uji' Bukoba inavyopiga pasi afya za watoto wake**

KIGOMA KUNA MAMBO...

**Balaa lililojificha wajawazito wa mkoa wang'ang'ania dawa pori za uchungu**

Ukurasa 13





Ukurasa 14

**Mkakati wa RC Kunenge kuitakatisha Dar kimazingira, isahau kipindupindu**

# Neno rasmi la Wizara Afya, dawa asili zilipotua mtaani kuchuana na 'yajayo'

**Na Yasmine Protace**

HIVI karibuni serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, iliweka mkakati wa kusogeza karibu huduma za tiba asili kwa jamii.

Ni aina ya dawa ambazo zinawekewa mikakati ya kupatikana hadi kwenye vituo vya kutoa huduma za afya na maduka ya kuuza dawa za binadamu.

Mganga Mkuu wa Serikali, Profesa Abel Makubi, anawaambia wazalishaji dawa asilia nchini, baada ya kikao na wazalishaji dawa hizo ambako zimethibitishwa usalama na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Msajili wa Tiba Asili nchini, kukidhi vigezo vya kutumika kwa binadamu.

"Sisi watendaji tumeona ni muhimu kukutana ili tuweze kuweka mikakati ya kuhakikisha hizi dawa asili zinawafikia wananchi kwa urahisi zaidi," anafafanua Prof. Makubi.

Anasema jamii inasumbuliwa na magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza, hivyo ni lazima kutumike silaha (dawa asilia na za kisasa) zote salama zinazoweza kuwasaidia wananchi kwa afya.

"Kuna hizi dawa asili zenye usalama ambazo zimekuwa zikitumika kutibu magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambikiza, hivyo ni lazima tuzisogeze karibu kwa wananchi kupitia wakala, maduka ya dawa ya binadamu nata hospitalini kwa usalama ziweze kuwafikia wananchi" anasema.



Wazalishaji dawa asilia na wataalamu wa afya ,wakiwa kwenye kikao cha kujadili namna bora ya kurahisisha upatikanaji dawa asilia ndani ya jamii. Picha ndogo duara, ni Mganga Mkuu wa Serikali, Profesa Abel Makubi. **PICHA: YASMINE PROTACE.**

Rai ya Mganga Mkuu wa Serikali, anawataka wasomi na wataalamu wa afya kwa ujumla, kubadili mtazamo wao kuhusiana na tiba asili, kwa kuwa zina mchango mkubwa wa kutibu magonjwa ya binadamu.

Anawaasa wataalam wa afya, kutokuwapa vikwazo wananchi katika utumiaji wa tiba asili, akiwa na ufafanuzi:

"Kama dawa sisi tumeshaihakiki na tukaikubali kwamba hii dawa ni salama, basi pasiwapo kinyongo au ugumu wowote wa sisi watumishi wa afya kuruhusu mwananchi kutibiwa kwa dawa hiyo."

Pia, hakusita kuwaasa wananchi waendelee kuchukua tahadhari za kinga za magonjwa yote, ikiwamo ufanyaji mazoezi, kubadili mtindo wa maisha na kula chakula bora, kwa mujibu wa maelekezo ya kidaktari.

Prof Makubi anaelezea pia umuhimu wa kufanyika utafiti zaidi wa tiba asilia, ili ziweze kuhakikishwa kwa miongozo ya nchi na kimataifa na baadaye kuweza hata kuhudumia wananchi wa nchi za jirani.

Aidha anasisitiza wagunduzi kwamba watalindwa na serikali na kuhakikisha umiliki wa ugunduzi wa dawa hizo haupotei wakati na baada ya utafiti.

**MKURUGENZI TIBA ASILI**

Dk. Paul Mhame, Mkurugenzi Msaidizi waa Tiba Asili kutoka Wizara inayohusika, anasema kupitia taasisi zake, imechambua na kuidhinisha aina tano za dawa za kunywa na dawa aina nne za mafuta tete kwa ajili ya kujifukiza, zilizokidhidi vigezo kutumika kwa binadamu.

Anazitaja dawa hizo za kunywa kwa majina ya kitaalamu: NIMRICAF; COVIDOL; BINGWA; PLANET ++; na COVOTANZA na Dawa kutoka jamii ya mafuta zinaitwa BUPIJI na UZIMA.

"Serikali inaendelea kufanya kazi kwa karibu na wazalishaji wengine ambao wakikidhi vigezo dawa zao zitaongezwa kwenye orodha hii," anasema

Dk. Mhame anawasisitiza wananchi kujitokeza kwenda kununua dawa hizo kwa ajili ya kujikinga na magonjwa ambukizi na yasiyoambukiza.

**WAGUNDUZI WAANIKA**

George Buchafwe, anasema wametengeneza dawa ya kujifukiza kwa mafuta tete ya Bupiji, kwa niaba wenzake anaishukuru serikali kuwa na maono kuwa sehemu ya kuchangia na kuboresha afya za wananchi. Buchafwe, anafafanua:

"Tunaishukuru serikali kwa kutambua kuwawapo watafiti ambao wanaweza wakaisaidia jamii yetu na ikawezakutoka katika hatua kwenda hatua nyingine kwa kutumia tiba zetu za asili.

Anasema kuwa wao wazalishaji wa dawa za asili, wapo tayari kushirikiana na serikali kuzalisha bidhaa bora yenye usalama kwa afya ya binadamu.

Kwa upande wake Dk. Joseph Otieno, kutoka Taasisi ya Tiba Asilia Muhimbili, anasisitiza umuhimu wa wananchi kuacha kuchanganya dawa zaidi ya moja kwa wakati moja wakati wa kutumia.

Pia, anahimiza haja ya wa kufuata maelekezo sahihi ya matumizi ya dawa wanazopewa na kuzingatia usalama wake.

AFYA

# Jitihada za 'Operesheni Uji' Bukoba inavyopiga pasi afya za watoto wake

## • Shule 22 wanachama, mbili njiani



Wananfunzi wa shule za Manispaa ya Bukoba, katika nyendo zao kupata mlo. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Lilian Lugakingira, BUKOBA**

MANISPAA ya Bukoba imo katika orodha ya halmashauri nchini zenye utaratibu wa shule zake za msingi za serikali kutoa huduma ya mlo uji, ili kulinda afya za watoto na kuongeza ufaulu.

Ofisa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi, anayeshughulikia Afya, Lishe na Usafi wa Mazingira katika Shule za Msingi na Sekondari katika manispaa hiyo, Florance Kibani, anasema kuna shule 22 za serikali zenye huduma ya uji kati ya 25 zilizopo.

Anasema, katika orodha hiyo kuna shule mbili maalumu anaozitaja kuwa ni Mugeza Mseto na Mugeza Viziwi, zenye ziada ya kutoa chakula kutokana na aina ya watoto wanaosoma mahali hapo.

Katika kipindi cha mlipuko wa ugonjwa COVID 19 mwaka jana, serikali ilitangaza kufungwa shule zote ili kudhibiti maambukizi na baada ya ugonjwa kupungua, serikali iliruhusu shule kufunguliwa.

Hapo ulitolewa utaratibu wa kuongeza muda wa masomo kutoka saa 8:30 mchana hadi saa 11.00 jioni, lengo ni kufidia muda uliopotea baada ya shule kufungwa kutokana na mkasa maradhi corona. Baada ya muda mfupi ulisitishwa na kutafutiwa mbadala.

Anasema, walikubaliana kubadilisha muda wa kuanza vipindi, badala ya kuanza saa 2:00 asubuhi walianza vipindi saa 1:30 na kufanya muda wa kuruhusu watoto kurudi nyumbani kubakia saa 8:30 mchana.

"Pia, tulipunguza muda wa mapumziko, kwa mfano walikuwa wanapumzika nusu saa, walianza kupumzika kati ya dakika 15 hadi 20 na muda uliokombolewa ulitumika kufundisha" anasema.

Florance anasema utaratibu huo umewezesha kutowakalisha watoto shuleni muda mrefu ili kulinda afya zao, hasa watokao katika shule tatu zisizo na huduma za uji shuleni.

Katika hilo, walimu wanatumika kuwahamasisha wazazi kuwafungia watoto vyakula kidogo, vinavyowasaidia kupunguza njaa shuleni.

"Baadhi ya wazazi huwapa watoto wao hela ambazo hununua vitu kulingana na hela aliyopewa mtoto, lakini jitihada za kuwahamasisha wazazi na walezi kuchanga hela ya uji shuleni zinaendelea, ili shule zote 25 za serikali ziwe na huduma hiyo," anasema.

Anasema, hivi sasa wamejipanga kuitisha mikutano ya wazazi shuleni kuweka mikakati ya pamoja katika shule zisizo na huduma, nazo ziweze kuanzisha, huku wao maofisa wako mstari wa mbele kuhudhuria na kuhamasisha lengo. "Tumejipanga kushirikiana na waheshimiwa madiwani, wenyeviti wa serikali za mitaa na watendaji, kwa kushirikiana na maofisa elimu kata, walimu wakuu na walimu wa afya na lishe" anasema.

**MADHARA YA KUKOSA MLO**

Ofisa huyo anayeratibu mkakati, anataja madhara yanayoweza kuwakumba watoto wanaoshinda na njaa, pasipo kupata walau uji wakiwa shuleni, anataja ni hatari kuongezeka utoro wa rejareja.

"Inapofika muda wa mtoto kuhitaji kuweka chochote tumboni, kama hakipo watoto hutoroka na kwenda nyumbani na baadae kurudi shuleni, wakati mwingine kuna masomo huwapita," anasema na kuongeza:"Pia kuna mtoto mwingine kama kwao ni mbali, akiondoka harudi shuleni."

Florance anaeleza kukosa mlo, pia kunawajengea baadhi ya watoto tabia ya kutorudi nyumbani wakitoka kula, wanakimbilia ashamba ya watu kuiba vyakula kama mihogo, miwa na maembe na ndio mwanzo kujifunza wizi katika umri mdogo.

Pia, Florance anasema kiafya inachangia mtoto kupata saratani ya utumbo, kwa sababu anapokaa darasani muda mrefu pasipo mlo, utumbo una kawaida ya kujisokota na kuishia vidonda, hadi mwisho wake ni saratani ya tumbo.

Kingine anakieleza:"Usikivu darasani pia hupungua, mwalimu anapokuwa anafundisha mtoto mwenye njaa, kinachowasilishwa hawezi kuelewa vizuri, maana anawaza ama uji au chakula" anasema.

Kingine anachokitaja ni kuharibika uhusiano wa kijamii, unaendana na utengano kati ya mtoto anayepata uji au chakula shuleni na asiyeambulia chochote cha kula.

Ofisa Florance anafafanua: "Asiyekula ama kunywa uji ataanza kuonekana maskini zaidi na kubaguliwa shuleni."

**HATUA ZINAZOCHUKULIWA**

Anasema, ili kukabiliana na changamoto hiyo kuna Waraka wa Elimu Namba Sita wa Mwaka 2015, unaoainisha majukumu ya serikali kuu, halmashauri, wazazi na mwanafunzi, uliosambazwa katika shule kupitia kwa walimu wakuu na maofisa elimu kata.

Ni waraka unaoainisha haja ya wazazi kugharamia mahitaji mbalimbali ya wanafunzi kama sare na vifaa hitajika, pia chakula na matibabu kwa wanafunzi wa kutwa kwa watoto wao.

Kutokana na maelekezo yaliyoko katika waraka huo, walimu na maofisa elimu, wana wajibu wa kuendelea kutoa ufafanuzi kwa wazazi na walezi kuhusu wanayopaswa kutekeleza, ikiwamo kugharamia chakula au uji kwa wa watoto wao wakiwa shuleni.

"Ilikwishaitishwa mikutano ya wazazi na idara (Elimu) husika tukaenda kufafanua huo waraka kuhusiana na umuhimu wa mtoto kula au kunywa uji shuleni na jukumu la mzazi kwa mtoto anayesoma," nina imani elimu hii itaendelea, ili kuhakikisha shule zote zinatoa huduma hiyo" anasema.

**DOKEZO LA WAZAZI**

Vicencia Patience, mzazi anayeishi eneo la Kyakailabwa, Manispaa ya Bukoba, anasisistiza umuhimu wa mtoto kupata uji au chakula shuleni, kwani ni kioo cha kumuweka sawa mtoto kiafya, huku ikimsaidia kufanya vizuri katika masomo shuleni.

Anaelezaa udhaifu wa kijamii uliopo, wazazi wengi wanashindwa kuamka mapema kuwaandalia chai watoto kabla ya masomo, hivyo ni vigumu kwao kuvumilia njaa kuanzia mapema asubuhi saa 1:30 hadi saa 8:30 mchana anapotoka kurudi nyumbani.

"(Baadhi ya wazazi) Hawawajali watoto wao, mzazi analala tu hafuatilii kama mtoto wake ameweka chochote tumboni kabla ya kwenda shule. Hii sio haki wanapaswa kubadilika," anasema

Mama huyo ana upande wa pili ni kwamba, akikiri kwamba kuna shinikizo la hali ya kiuchumi kwa badhi ta wazazi, haiko sawa.

Aidha, Mama Vicencia, anatumia fursa hiyo kuomba itumike mikutano ya serikali za vijiji na mitaa kuwaelimisha wazazi na walezi, umuhimu wa kuwaandalia chai watoto kabla ya kwenda shule na umuhimu wa kuchangia fedha za kuwawezesha kunywa uji shuleni.

Pamoja na tatizo la COVID 19 lililosababisha ratiba ya masomo kubadilika, bado wanafunzi wameonekana kufanya vizuri katika mkoa wa Kagera katika matokeo ya mtihani wa taifa wa darasa la saba mwaka huu.

**YANATOKANAYO JE?**

Kuna matunda kupitia picha ya jumla ya waliofanya mtihani mkoani Kagera walikuwa 51,457 na waliofaulu 45,427 sawa na asilimia 88.28, Manispaa ya Bukoba iliyoko katika 'operesheni uji' ikishika nafasi ya kwanza.

Hiyo inafanyika, huku Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watoto wa Mwaka 1989 unazitaka nchi wanachama ikiwamo Tanzania, kutambua haki ya kila mtoto kuwa na kiwango cha maisha kinachokidhi makuzi ya kimwili, kiakili, kiroho, kimaadili na kijamii.


Pia, wanachama wanatakiwa kulingana na hali zao kitaifa na uwezo wachukue hatua zinazofaa kuwasaidia wazazi wahusika na wengine na mtoto kutekeleza utoaji msaada wa mali, kusaidia mipango inayohusu lishe, mavazi na makazi.

AFYA

KIGOMA KUNA MAMBO...

# Balaa lililojificha wajawazito wa mkoa wang'ang'ania dawa pori za uchungu

- Wakiingia 'leba' wanazo kwa siri
- Mbinu kuu wanadumbukizia chai
- Wanaofanya wafunguka siri kuu




Ofisa Muuguzi Msaidizi wa Kituo cha Afya Ujiji kilichopo manispaa ya Kigoma Ujiji, Dk. Kamuli Kazinza, alipoelezea namna wanavyowabaini wajawazito wanaotumia dawa za kienyeji kuongeza uchungu wakati wa kujifungua. **PICHA: PENDO THOMAS.**

**Na Pendo Thomas, KIGOMA.**

UJAUZITO huwa unabeba mana moja tu. Ni hali ya mwanamke kuwa na kiumbe kinachoendelea kukua kwenye mfuko wake wa uzazi wake hadi kukomaa na anajifungua katika wastani uliozoeleka, miezi tisa.

Watalamu wa afya wanashauri, katika kipindi hicho mjamzito anapaswa kuongeza umakini katika maisha ya kila siku, ikiwamo kuzingatia ushauri wa kitaalamu na kuepuka matumizi ya aina zote za dawa, pasipo maelekezo ya kidaktari.

Ni umakini utakaomsaidia kuepuka madhara ya kiafya na tumboni mwake, mpaka anapojifungua.

**KIGOMA KULIVYO**

Baadhi ya wanawake wa mkoani Kigoma, wamekuwa wakitumia dawa za kienyeji ambazo hazijathibitishwa katika kipindi cha ujauzito, hasa wanapokaribia kujifungua.

Mtaalamu bingwa wa magonjwa ya uzazi ya kinamama kutoka Hospitali ya Kamanga, jijini Mwanza (Kamanga Medics Center) Dk. Anthony Masinde, anasema utumiaji dawa za kienyeji kwa wajawazito, hatari yake kiafya inamuagukia mama na kiumbe alicho nacho tumboni.

Anaweka shaka ya dawa hizo zina uwezo wa kusababisha mimba kutoa mtoto mwenye matatizo ya kimaumbile na hata matukio ya vifo, ikiwamo ya mama.

Daktari anasema dawa zinazohitajika ni zilizofanyiwa tafiti na kuonyesha kiwango cha dozi inayopaswa kutumiwa na mwanamke mjamzito, pamoja na aina ya kiwango cha kemikali ndani ya dawa husika.

"Ubaya wa dawa nyingi za kienyeji zinazotumika hazijafanyiwa tafiti, wala mtu hajui mchanganyiko wake una aina ngapi ya kemikali hii ni hatari," anasema Dk. Masinde.

**HATARI ILIYOJIFICHA**

Huenda vitendo hivyo vimekuwa vikichangia ongezeko la vifo vya wanawake wajawazito na watoto wachanga mkoani humo na Tanzania, licha ya kazi kubwa inayofanywa na Serikali kuboresha huduma za uzazi kwa wanawake ikiwemo uhimizwaji wa matumizi ya uzazi wa mpango.

Ripoti ya Idadi ya Watu na Afya (DHS) ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ya Mwaka 2015/16 inaonyesha mwaka huu, viliripotiwa vifo 556 vya uzazi katika kila vizazi hai 100,000, ni idadi kubwa, lakini haijafikia kilichojiri katika mwaka 2004/05 waliokuwa

**KINAMAMA 578.**

Katika siku za karibuni ya mwaka 2012, vilikuwapo orodha ya vifo 432 vitokanavyo na matatizo ya uzazi.

Katika Mkoa wa Kigoma, mwaka jana walifariki wanawake 119 kutokana na sababu mbalimbali, kwa mujibu wa takwimu za Mfumo wa Huduma za Afya (Health Infomation System), iliyotolewa na Mratibu wa Afya ya Uzazi na mtoto mkoa wa Kigoma, Ernest Teyumwete.

Idadi hiyo ya vifo hivyo ni ongezeko la idadi 19 kutoka vifo 100 vilivyorekodiwa mwaka 2019 katika kipindi cha mwaka mmoja.

Ni hali inagharimu uzazi na uhai wa watoto wachanga wanaozaliwa mkoani humo, kwa sababu mama zao wameshindwa kufuata taratibu za afya kama inavyopendekezwa.

Kurejea takwimu zilivyo, kuna ongezeko la vifo vya watoto wachanga mkoa Kigoma, hali ambayo Mratibu, huyo wa Afya ya Uzazi na Mtoto, anasema kuna hatua za udhibiti zinachukuliwa kukabili hilo.

**WAHUDUMU WASHITUKA**

Licha ya kunywa dawa za kienyeji miongoni mwa wajawazito wa Mkoa wa Kigoma kufanyika kwa siri, sasa vimeanza kujidhihirisha kwa wahudumu wa afya.

Muuguzi katika Kituo cha Afya cha Ujiji mkoani hapa, Kamuli Kazinza, anathibitisha kushuhudia vifo kwa miaka katika kituo hicho cha afya vinayohusiana na matumizi ya dawa za kienyeji za kuwaongezea uchungu wajawazito.

Anasimulia mkasa wa mwanamke aliyefika kituoni kujifungua alipokunywa chai kama ilivyo kawaida ya ushari kwa wajawazito wanaokaribia kujifungua, ndipo muuguzi alibaini kuwapo mzizi wakati mama huyo akisaidiwa kumiminia chai kwenye kikombe .

"Kuna wakati mjamzito anaweza kuja akiwa amechanjwa chale tumbo zima au amepaka majani ya kijani tumboni," anasema muuguzi huyo na kubainisha, wapo wanaopatwa na uchungu uliopitiliza.

Ofisa Muuguzi kutoka Hospitali ya Wilaya ya Baptist mkoani Kigoma, Robert Tondiye, anasema matumizi ya dawa hizo hubainika mjamzito anapopata hali isiyo ya kawaida kabla ya kujifungua.

Anafaanua kuwapo, uchungu mkubwa wa mjamzito ndani ya muda mfupi na wapo wanaotoa damu nyingi.

Tondiye anasema, ni hali inayoathiri ufuatiliaji wa mwenendo wa uchungu, kwani kwa kawaida mjamzito anapaswa kupimwa mara tatu hadi nne, kukagua njia ya kupitisha mtoto.

"Kutokana na dawa hizo, baadhi ya watoto hulazimisha kutoka kabla ya njia kuongezeka, hivyo kusababisha ulazima wa upasuaji ili kuokoa maisha ya mama na mtoto... wakati mwingine vifo hutokea," anaeleza.

Sera ya Afya ya Taifa ya Mwaka 2007, inaeleza umuhimu wa kuongeza juhudi katika za utoaji huduma, ili kudhibiti vifo vya wajawazito na watoto wachanga.

Kimsingi, inaielekeza serikali kwa kushirikiana na wadau, iboreshe miundombinu zinazowawezesha wajawazito na watoto wachanga kufikiwa na kuzitumia huduma za afya.

**KINAMAMA WAONGEA**

Amina Shaban (Si jina halisi), ni mkazi wa Manispaa ya Kigoma Ujiji, ambaye sasa ni mjamzito, anasema ana dawa ya kienyeji anayoitumia kipindi cha ujauzito, ili kusaidia 'anachokiita' ukuaji wa mtoto tumboni.

"Dawa hii inamkinga mtoto na maambukizi mengi, hata pale mwanaume anapotoka nje ya ndoa, mtoto hawezi pata madhara tumboni," anasema.

Mama huyo wa watoto sita, anadai anapopata uchungu wakati wa kujifungua, hutumia dawa hiyo akiwa nyumbani au hospitali kwa siri, familia yake humuwekea kwenye chupa ya chai na anaendelea kuinywa pasipo watoa huduma za afya kumbaini.

Anasema, dawa hizo za kienyeji humsaidia asikae hospitali muda mrefu, akisubiri kujifungua na ndani ya saa chache anapofika sehemu ya kutoa huduma za afya, anapata uchungu mkali na baadae kujifungua.

Licha ya kutumia dawa hizo kila anapopata ujauzito, anakiri amekuwa akitokwa na damu nyingi wakati na baada ya kujifungua, jambo ambalo limeweka rehani maisha yake mara kadhaa.

"Baada ya kujifungua huwa ninatokwa na damu nyingi sana lakini naamini hiyo ni hali ya kawaida kwa ababu wanawake tunatofautiana maumbile," anasema Amina.

Neema John (si jina halisi), mwenye umri wa miaka 44, mkazi wa Manispaa ya Kigoma Ujiji, anasema alipopata ujauzito wa pili akiwa mkoani Rukwa, alipatiwa dawa na mwanamke mmoja aliyemuelekeza inapaswa kutumiwa ujauzito unapofikisha miezi minane.

Neema anasema, inamsaidia kutopitiliza tarehe stahiki ya kujifungua na inamuepusha kupata uchungu taratibu, hali inayoweza kumfanya akae muda mrefu hospitalini.

"Dawa hiyo ukifuata masharti ni nzuri sana, japo imekuwa ikitumika kutoa mimba, endapo ukiinywa mimba ikiwa changa," anasema, mama huyo wa watoto wanane.

Nini kifanyike? Mratibu Teyumwete, anasema ''Tutaendelea kutoa elimu ya kupinga matumizi hayo hadi pale jamii itakapotambua madhara ya dawa za kienyeji kwa wajawazito," anasema Teyumwete.

AFYA

# Mkakati wa RC Kunenge kuitakatisha Dar kimazingira, isahau kipindupindu

## •Hatua nini kifanyike imekaa mezani
## •Tabibu bingwa: Huu hapa mchakato



Wahudumu afya wakipambana na kipindupindu katika jukumu la usafi.

**Na Sabato Kasika**

KIPINDUPINDU ni ugonjwa unaoathiri jamii maskini zaidi, hasa walioko katika nchi zinazoendelea na wataalamu wa afya wanasema, kinapatikana katika vyanzo kama vyakula, maji machafu na kinyesi kutoka mtu kwa aliyeambukizwa au vyanzo vya asili na chanzo kikubwa cha kinatajwa kuwa uchafu.

Hivyo, inaepookea jamiii itazingatia usafi, basi mlipuko wa kipindipindu una kawaida kukumba baadhi ya maeneo, mahsusi katika mikoa mbalimbali, ikiwamo Dar es Salaam.

Tayari uongozi wa mkoa huo unasema, umekuja na mikakati mbalimbali ya kudhubiti tatizo la uchafuzi wa mazingira, ikiwa ni pamoja na kila mkazi kusafisha mazingira ili kukabiliana na magonjwa ya mlipuko.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge, anasema katika timu yake wamejipanga kukifanya, anataja mikakati mengine ni kutumia kampuni ya usafi ya umma, kufanya usafi kwenye baadhi ya maeneo ya jiji.

"Mikakati mingine ni manispaa za jiji kuongeza adhabu kwa wanaotapisha majitaka kwenye makazi na mitaro ya maji ya mvua na pia tutaboresha dampo za taka," anasema Kunenge.

Anafafanua kuwa mkoa Dar es Salaam, hivi sasa una mkakati wa kujenga kiwanda cha kuchakata taka na kuzigeuza kuwa mbolea, upandaji miti, na utunzaji bustani kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, zikiwamo benki kubwa za nchini.

'Kwa ujumla ni kwamba, tumejipanga kuzipatia ufumbuzi kero mbalimbali wananchi, ikiwamo uboreshaji wa huduma za afya, elimu, maji na kuweka mazingira bora," anasema.

**KUAMBUKIZWA KULIVYO**

Daktari bingwa wa magonjwa ya binadamu, Lucas Nzobendo, kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), ana fafanua: "Adui wa ugonjwa huo ni usafi, kwani unatokana na maambukizo katika utumbo mdogo wa binadamu na unaletwa na vimelea vya bakteria ambavyo kitaalamu vinaitwa 'vibrio cholera.

"Vimelea hivyo vina kawaida ya kupendelea kuishi katika kinyesi cha binadamu na katika hilo, mtu anaweza kuambukizwa kwa kunywa maji au chakula kilichochafuliwa na kinyesi chenye vimelea hivyo vya kipindupindu na anaishia kuugua.

"Mara baada ya kula chakula au kunywa maji yaliyochafuliwa, baadhi ya vimelea hivyo huuawa kwa tindikali iliyopo kwenye tumbo, wakati chakula au maji yanapoingia tumboni."

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, baadhi ya vimelea vinaweza kukwepa makali ya tindikali hiyo na kuendelea kuishi kwa kujongea hadi kuufikia ukuta wa utumbo mdogo wakitumia 'maumbo' maalum yaliyo katika miili yao yanayowezesha kusafiri na kitaalamu anayataja kwa jina 'flagella.'

"Wanapokuwa kwenye ukuta wa utumbo mdogo (Vibrio cholerae), hutoa sumu iitwayo CTX au CT (cholera Toxin) ambayo husababisha mtu kuharisha choo chenye majimaji," anasema Daktari

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, athari za kipindipindu huendelezwa kutolewa nje kwa njia ya kinyesi cha haja kubwa na kwa mtu aliyeambukizwa kipindupindu kinapochanganyika na chanzo cha maji au chakula, athari huenda kwa watu wengine wanaoambukizwa kirahisi.

Ni athari inayotawala zaidio penye choo kisicho na mazingira safi, nacho kina hatari ya kuambukizwa kuchanganyika na chanzo cha maji au chakula, hivyo kusababisha watu wengine zaidi kuambukizwa kipindupindu.

**UCHAFU WA JIJI**

Mtaalam Mshauri wa Masuala ya Mazingira na wa Mipango Miji, kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Dk. Hussein Omari, anasema, Dar es Salaam inakadiriwa kuzalisha zaidi ya tani 4,600 za taka kwa siku.

Anasema, hizo kumbukumbu rasmi alizo nazo ni kwamba, kati ya asilimia 45 hadi 50 ya taka zinazopokelewa dampo, ambayo kwa uzito ni wastani wa tani 1,200 hadi 2,000 ya taka zinazozalishwa kwa siku, huku kiasi kingine cha taka kati ya tani 3,400 na tani 2600 zinaishia katika maeneo ya wazi, mitaro ya maji, barabara na makazi ya watu.

"Udhibiti taka ngumu ni tatizo la muda mrefu, kwani ni tabia iliyozoeleka miongoni mwa jamii ya utupaji taka ovyo katika maeneo yasiyostahili imechangia jiji la Dar es Salaam kuwa chafu," anasema Dk. Omari.

Mtaalam huyo wa mazingira anasema, kuzagaa kwa taka ni kichocheo cha milipuko ya magonjwa kikiwamo kipindupindu na mengine ya kuhara na kutapika.

"Kimsingi hali hiyo ya uchafu inachangiwa pia na elimu ndogo juu ya usafi wa mazingira, kutotii sheria zilizopo kwa upande wa wananchi na usimamizi hafifu wa sheria za usafi wa mazingira," anasema.

**NINI KIFANYIKE?**

Dk. Omari anasema, jiji la Dar es Salaam lina kinachoitwa Sera ya Urejelezaji wa Taka Ngumu, ikilenga kuzisaidia taasisi za serikali kutambua na kurasimisha sekta hiyo tajwa, ambayo awali iliendeshwa na taasisi binafsi na vikundi visivyo rasmi.

"Kwa kutumia sera hiyo, uchafuzi wa mazingira unaweza kupungua, kwani viongozi wanaweza kubuni miradi mbalimbali inayolenga urejelezaji taka pamoja na masoko ya uhakika ya taka zilizorejelezwa," anasema.

Dk. Omari anasema, jamii pia inatakiwa kuhamasishwa juu ya umuhimu wa kurejeleza taka, ikiwa ni pamoja na kushirikiana na halmashauri za manispaa katika utenganishaji taka unaofanyika kuanzia ngazi za uzalishaji.

"Vilevile ni muhimu kuwatambua na kuwaunganisha wadau mbalimbali wanaojihusisha na teknolojia za urejelezaji taka jijini na kutenga maeneo ya viwanda vidogovidogo au karakana ndani ya dampo ama kuwa na maeneo yake ambayo yatafaa kwa kazi zinazohusiana na urejelezaji taka," anasema.

Anataja hatua kuwa inaweza kusaidia ukuaji wa sekta ya urejelezaji taka ngumu, kwa kuongeza viwanda na ubora wa bidhaa zake ili kupata soko ndani na nje ya nchi na hatimaye kukuza pato jamii na taifa.

"Wananchi wa maisha ya chini wakiwamo vijana na wanawake wanaweza kushiriki katika ubunifu na utumiaji wa teknolojia za urejelezaji taka na hatimaye kuboresha usafi," anasema.

Mtaalam huyo wa mazingira anasema, urejelezaji taka una faida nyingi katika jamii, ikiwamo kuongeza thamani ya taka na kipato cha jamii, kupunguza malundo ya taka katika mitaa na maeneo mbalimbali.

"Hatua hiyo pia hupunguza gharama za uendeshaji wa dampo, kupunguza gharama za udhibiti taka na kuongeza uelewa wa jamii katika uchambuzi wa taka kuanzia ngazi ya kaya," anasema.



Mazingira yaliyo rafiki kwa kipindupindu. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



## Machinga watakiwa kuziheshimu sheria

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

VIONGOZI wa machinga Mkoa wa Dodoma wametakiwa kutoa ushirikiano kwa serikali katika kuwasimamia wafanyabiashara ndogo, ili waweze kuheshimu sheria na kanuni zilizotolewa na halmashauri za jiji.

Rai hiyo ilitolewa na Mwenyekiti msaidizi wa umoja wa machinga Mkoa wa Dodoma, Bruno Mponzi, alipokuwa akizungumza na viongozi wa machinga kwenye kikao cha pamoja cha mpango kazi kati yao na ofisa masoko wa jiji la Dodoma.

Mponzi, aliwataka viongozi hao kuhakikisha wanawasimamia wafanyabishara ndogo kwenye maeneo yao ili wasiwe kikwanzo kwa serikali kwa kufanya biashara maeneo ambayo siyo rasmi.

Aidha, aliwataka viongozi hao kuhakikisha maelekezo yanayotolewa na serikali kupitia halmashauri husika hayakiukwi, badala yake wafanyabishara hao wafanye biashara zao maeneo ambayo yaliyotegwa rasmi.

Pia, aliwataka viongozi hao kuwa waelimishaji kwa wafanyabiashara wanaowasimamia kwa wale ambao bado wamekuwa kikwanzo kwa serikali.

Ofisa masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, akizungumza na viongozi hao wa machinga kwenye kikao hicho, aliwataka kutokuwa kizingiti cha kukwamisha maenedeleo ya wafanyabishara wanaowasimamia, badala yake watoe ushirikiano na halmashauri za miji na jiji.

Alisema viongozi wa machinga hawapaswi kuwa kero kwa halmashauri zinazowasimamia badala yake wanatakiwa kufanya kazi kwa kushirikiana.

"Mimi kama Ofisa masoko, halmashauri ya jiji inawategemea nyinyi viongozi wa machinga kuwaona wafanyabiashara hao ndogo ndogo wanaheshimu kanuni, sheria na maelekezo, ili wasiwe kikwanzo kwa serikali ukizingatia hivi sasa wamepewa uhuru wa kufanya kazi, lakini pia wanatakiwa kuzingatia miiko ya biashara," alisema.

Aliwaonya wafanyabishara ambao wamekuwa wakikiuka maelekezo kwa kufanya biashara zinazohatarisha usalama wa wateja kama vile wanaochoma mishikaki, kukaanga chipsi na samaki kwenye stendi za daladala.

Alisema biashara kama hizo kufanyika kwenye stendi zinaweza kuhatarisha maisha ya watu, hivyo hawapaswi kuwamo kwenye maeneo hayo kwa kuwa ni hatari yanapoweza kutokea majanga ya moto.

# Waziri, wadau sekta ya nguo wateta

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

NAIBU Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, amefanya mazungumzo na wadau wa sekta ya nguo na mavazi ili kusikiliza kero wanazokutana nazo, na mapendekezo yao katika kuboresha na kukuza sekta hiyo.

Akizungumza na wadau hao katika kikao hicho, Naibu Waziri huyo, aliwaagiza kuwasilisha kero walizonazo na rasimu za mipango mikakati ya kuboresha na kuendeleza viwanda na biashara katika sekta hiyo ili kukuza uchumi wa nchi.

**"Wafanyabiashara wanaoagiza nguo na mavazi kutoka nje hususan vitenge kufanya biashara kwa karibu na wenye viwanda vinavyozalisha nguo na mavazi katika kuboresha ubora wa nguo ili kukidhi mahitaji ya soko," alisema.**

Alisema hatua hiyo inalenga kuzalisha nguo na mavazi ya kutosheleza mahitaji ya ndani na kuuza nje ya nchi.

"Wafanyabiashara wanaoagiza nguo na mavazi kutoka nje hususan vitenge kufanya biashara kwa karibu na wenye viwanda vinavyozalisha nguo na mavazi katika kuboresha ubora wa nguo ili kukidhi mahitaji ya soko," alisema.

Aliagiza wenye viwanda vinavyozalisha nguo na mavazi kuongeza uzalishaji wa nguo bora na zenye viwango.

Hata hivyo, alisema sekta hiyo ndio sekta inayotoa ajira nyingi za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa wananchi.

Alisema Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali katika kuendeleza sekta ya nguo na mavazi nchini ikiwamo kukuza soko la ndani la bidhaa hizo pamoja na kuandaa na kutekeleza mkakati wa kuendeleza sekta ya pamba nguo hadi mavazi (Cotton to Clothing Strategy C2C 2016 - 2020 ) na kuuhuisha ambapo utekelezaji wake utaanza mwaka 2021-2032.

Katika kikao hicho kilichojumuisha wadau ambao ni watengenezaji na waagizaji wa nguo na mavazi kutoka nje ya nchi, waliwasilisha kero na mapendekezo yao kwa Naibu Waziri ili kuboresha na kukuza sekta hiyo.



Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe (katikati), akizungumza na wadau wa sekta ya nguo na mavazi alipokutana nao jijini Dodoma jana, ili kisikiliza changamoto wanazokutana nazo katika uendelezaji wa viwanda na biashara ya nguo na mavazi nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# BAKWATA yakataza migogoro misikitini

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

MWENYEKITI wa Halmashauri Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Wilaya ya Dodoma Mjini, Hussen Bashiru, amewataka mashekhe, maimamu na walimu wa madrasa kudumisha amani, upendo, umoja na mshikamano ili kuepusha migogoro ndani ya misikiti.

Bashiru, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na waumini wa msikiti wa Mtoro Maili mbili jijini Dodoma kwenye kikao cha pamoja kati ya viongozi wa wilaya BAKWATA na uongozi wa msikiti huo kwa ajili ya kutatua mgogoro uliodumu kwa miaka minne.

Akizungumza baada ya kuchaguliwa kwa viongozi watakaongoza kwa muda, Bahiru aliwataka kudumisha amani na mshikamano ili kuwajengea imani waumini wao ambao kwa kipindi chote wamekuwa kwenye migogoro.

Alisema migogoro inapotokea ndani ya misikiti inakwamisha shughuli zote za kidini, suala ambalo linapaswa kuzingatiwa ili lisije likawagawa waumini. "Leo tumefanikiwa kumaliza mvutano uliokuwapo ndani ya msikiti huu, kwa baadhi ya viongozi na waumini, ni mategemeo yetu sisi kama viongozi wa wilaya kuona na kusikia sasa mna maendeleo na viongozi wakidumisha amani na mshikamano kama Mtume wetu Mohamad (S.A.W) anavyotaka," alisema.

Naye Ustadhi Abas Abdalah, mzee wa msikiti huo, aliupongeza uongozi wa BAKWATA wilaya kwa kumaliza mgogoro na kuwaunganisha waumini wa msikiti huo ambao kwa miaka minne walikosa kuaminiana.

"Kwa kipindi cha miaka minne msikiti huu umegubikwa na wingu zito la mgogoro wa baadhi ya viongozi kutaka madaraka, hivyo ninawashukuru viongozi wa ngazi ya wilaya kwa kutatua na tunaamini sasa tutafanya kazi ili kuujenga upya msikiti wetu kiuchumi na kiroho," alisema.

Shekhe wa Baraza hilo Wilaya ya Dodoma, Hassan Kiza, aliwataka maimamu na walimu wa madrassa kuhakikisha wanafanya kazi ya dini ya kiislamu kwa mapana, umoja na kwa uelewi, badala ya kuchochea migogoro isiyo kuwa na tija.

Shekhe Kiza pia aliwataka viongozi wa msikiti wa Mtoro kujiepusha na migogoro kwa kuwa imekuwa ikikwamisha maendeleo ya waumini wa dini hiyo, badala yake watumie muda mwingi kudumisha na kuilinda amani na mshikamano. Imamu wa msikiti huo, Mohamed Nkusa, ambaye alikabidhiwa kuongoza baada ya kufanyika kwa uchaguzi wa viongozi wa mpito, aliuhakikishia uongozi wa Halmashauri ya BAKWATA wilaya kuondoa tofauti zilizokuwapo awali, nakwamba watasimamia kwa mujibu sheria na vitabu vitakatifu vya dini ya kiislamu.





# Mafuriko yasomba daraja, wananchi wakosa mawasiliano

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WAKAZI wa vijiji vitatu vya Kata ya Isuto katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wamekosa mawasiliano ya barabara, baada ya daraja la Mto Idiwili kusombwa na mafuriko yaliyosababishwa na mvua inayoendelea kunyesha wilayani humo.

Hali hiyo ilibainika juzi wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Wilaya hiyo ambayo ilitembelea miradi ya maendeleo ambapo wananchi walieleza kuwa vijiji vilivyokosa mawasiliano ni Isuto, Idiwili na Shisonta.

Mmoja wa wananchi hao, Fatuma Harrison, alisema kutokana na daraja hilo kukatika, wanashindwa kupata huduma muhimu za kijamii ambazo asilimia kubwa zinapatikana katika Mji Mdogo wa Mbalizi kutokana na usafiri wa magari kusitishwa.

Alisema tatizo hilo limekuwa sugu kwa maelezo kuwa awali lilijengwa daraja kubwa, lakini likaharibika hata kabla ya kuanza kutumika ndipo Serikali ikawajengea daraja la muda wakati ikijipanga kujenga la kudumu.

Alisema wakati wanaendelea kusubiri hata la muda lililojengwa likawa halipitiki kutokana na mto kujaa na kupitisha maji juu ya daraja hilo, hali iliyowafanya wamiliki wa magari waliokuwa wanatoa huduma kusitisha huduma.

"Kwa sasa hatuonani na wenzetu wa ng'ambo ya pili kwa sababu kama mnavyoona wamevunja kabisa daraja kubwa lililokuwapo hapa na hilo dogo limejaa maji, tunakosa huduma kwa sababu hatuwezi tena kusafiri kwa magari kwenda Mbalizi," alisema Fatuma.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Idiwili, Lingson Mtafya, alisema wananchi wake wanapata shida, hivyo akaiomba Serikali kuharakisha ujenzi wa daraja la kudumu ili mawasiliano yafunguke na wananchi wapate huduma.

Alisema kwa sasa kuna hatari ya baadhi ya wananchi kupoteza maisha endapo watatakiwa kwenda kutibiwa katika Hospitali ya Wilaya ama ya Rufani ya Mkoa kutokana na usafiri wa gari kutowezekana.

Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Mbeya, Hakimu Mwalupindi, alisema ujenzi wa daraja hilo ni miongoni mwa vipaumbele vilivyowekwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya chama hicho, hivyo akawataka wananchi hao kuwa wavumilivu wakati utekelezaji ukiendelea.

Alisema chama hicho kitahakikisha kinaisimamia Serikali ili itekeleze mradi huo kwa kiwango kinachotakiwa na kwamba daraja hilo ni muhimu kwa wananchi wa Kata hiyo kutokana na kwamba ndio njia pekee ya kufika Mbalizi.

"Kwa sasa naishauri Serikali ikiwezekana iongeze bajeti ya mradi huu ili yasije yakatokea kama yaliyotokea mwanzo, wananchi wa huku wanafanya kazi sana na ni wengi hivyo sisi tutaisimamia Serikali mpaka mwisho," alisema Mwalupindi.

Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) wa Wilaya ya Mbeya, Mhandisi Seleman Mziray, alisema mkandarasi wa kujenga daraja hilo alishapatikana na alianza kufanya baadhi ya kazi, lakini akalazimika kusimama baada ya mvua kuzidi.

Alisema kazi ya kwanza aliyofanya mkandarasi huyo ni kuvunja daraja la awali na kuanza kuchimba msingi, lakini ikabainika kuwa eneo hilo halina mwamba mgumu, hivyo akalazimika kusitisha kazi mpaka mvua itakapokuwa imepungua.

Mziray alisema daraja hilo linakusudiwa kujengwa kwa gharama ya Sh. milioni 229, na kwamba watasimamia ili kuhakikisha linajengwa kulingana na thamani halisi ya fedha hizo.



Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Kimondo, Kata ya Igoma, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wakiogesha mifugo yao kwenye josho la kata hiyo, hivi karibuni baada ya kupewa dawa za kuogesha bure na Serikali. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Mafundi simu kupewa fursa

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

MAFUNDI simu wameshauriwa kujiunga kwenye vikundi ili iwe rahisi kujengewa uwezo na taasisi mbalimbali zinazofanya kazi hiyo kulingana na mabadiliko ya teknolojia yanayotokea mara kwa mara.

Ushauri huo ulitolewa na Meneja wa Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Asajile John, wakati wa mkutano maalumu kati ya maofisa wa taasisi hiyo na mafundi wanaotengeneza simu.

Asajile alisema Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuhakikisha mawasiliano ya simu yanafanyika kwa usahihi ili kuepusha matatizo ikiwemo kusajili kadi zote za simu ambazo alidai ziko zaidi ya 49,000.

Alisema wameamua kuanza kutoa elimu hiyo kwa mafundi kutokana na baadhi ya mafundi hao kufanya kazi bila kufuata sheria na hivyo kusababisha matatizo kwenye mawasiliano.

"Undeni vikundi na ikiwezekana muwe na chama chenu ili tunapotaka kuwapatia mafunzo iwe rahisi kuwakuta kwa pamoja, teknolojia imekuwa ikibadilika mara kwa mara na hivyo ili kuendana na mabadiliko haya lazima nanyi tuwapatie mafunzo," alisema Asajile.

Alisisitiza kuwa kwa mujibu wa sheria kila fundi simu lazima awe na Leseni inayomruhusu kufanya kazi hiyo na kwamba vinginevyo hatua kali zitakuwa zinachukuliwa kwa mujibu wa sheria za mawasiliano.

Baadhi ya mafundi waliohudhuria mkutano huo walisema watahakikisha wanafanya kazi hiyo kwa kufuata sheria ili kuepuka kuchukuliwa hatua.

# Mhudumu afya ahukumiwa kuiba dawa, kuomba rushwa

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

MHUDUMU wa afya wa Hospitali ya Wilaya ya Kyela, Hilda Nsasu, aliyekuwa anatuhumiwa kuiba dawa na vifaa tiba vya hospitali hiyo pamoja na kuomba rushwa kwa wagonjwa, amehukumiwa kwenda jela miaka mitatu ama kulipa faini ya Sh. 1,000,000.

Mhudumu huyo alinaswa Desemba 17, mwaka jana na makachero wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Kyela akiwa na dawa na vifaa tiba mali ya hospitali hiyo kwenye mkoba wake na vingine akiwa amehifadhi nyumbani kwake.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, Julieth Matechi, baada ya uchunguzi kukamilika, taasisi hiyo ilimfikisha Nsasu katika Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Wilaya ya Kyela kwa ajili ya hatua za kisheria.

Alisema mahakama hiyo ilimtia hatiani kwa makosa mawili ya kuiba dawa na vifaa tiba na kuomba na kupokea rushwa kutoka kwa wagonjwa waliokuwa wanaenda kutibiwa hospitalini hapo.

"Mhakama imemhukumu kulipa Sh. 500,000 kwa kila kosa ama kwenda jela miaka mitatu kwa kila kosa, amelipa Sh. 1,000,000 kwa makosa yote na akaachiwa huru. Pamoja na adhabu hiyo, pia mahakama imetaifisha dawa na vifaa tiba alivyokuwa ameiba," alisema Matechi.

Alifafanua kuwa kosa la kuomba na kupokea rushwa ni kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa namba 11 ya mwaka 2007 na kwamba kosa la wizi wa dawa na vifaa tiba ni kinyume na kifungu cha 258 na 270 vya kanuni ya adhabu sura ya 16.

Alisema Disemba 17, mwaka jana maofisa wa TAKUKURU walimuita mhudumu huyo kwa ajili ya mahojiano baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya wagonjwa waliokuwa wanaenda kutibiwa wakimtuhumu kuwa alikuwa anawaomba rushwa.

Alisema wakati maofisa hao wanaendelea kumhoji walibaini alikuwa ameanza kuingiwa na wasiwasi, ndipo wakaamua kumpekua kwenye mkoba wake ambamo walikuta amehifadhi dawa mbalimbali za hospitali.

Matechi alisema maofisa hao waliamua kwenda kumpekua nyumbani kwake wakishirikiana na uongozi wa hospitali na ndipo wakakuta amehifadhi dawa na vifaa tiba vya hospitali nyumbani kwake.

Awali Mkuu huyo wa TAKUKURU alisema kwenye uchunguzi uliofanywa na maofisa wa taasisi hiyo, ilibainika baadhi ya watumishi wa Hospitali ya Wilaya ya Kyela wakiwamo madaktari sio waaminifu kutokana na kushirikiana na wahudumu kuiba dawa.

Alisema watumishi hao wamekuwa wakiiba dawa hizo kwa kutumia fomu za baadhi ya wagonjwa wanaotumia kadi za Mfumo wa Bima ya Taifa ya Afya (NHIF) waliowahi kwenda kutibiwa hospitalini hapo kwa kuzijaza upya ili ionekane watu hao walienda kutibiwa na kisha kuzitorosha dawa wanazojaza kwenye fomu.

# Wawakilishi wa ACT-Wazalendo waapishwa

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WAJUMBE watano wa Baraza la Wawakilishi kutoka Chama cha ACT-Wazalendo jana, walikula kiapo cha uaminifu mbele ya Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zuberi Ali Maulid.

Watatu ni wa majimbo ya uchaguzi kutoka Pemba ambao walishinda katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka jana na wawili waliteuliwa na Rais.

Wajumbe hao ni Nassor Ahmed Mazrui ambae pia ni Naibu Katibu Mkuu wa ACT Wazalendo na Omar Said Shabani ambae pia ni mwanasheria kutoka chama hicho ambao waliteuliwa na Rais.

Wengine ni Hassan Hamad Omar Mwakilishi wa Jimbo la Kojani Kisiwani Pemba, Habib Ali Mohammed kutoka jimbo la Mtambwe na Kombo Mwinyi Shekhe wa Jimbo la Wingwi.

Wajumbe hao baada ya kula kiapo walipongeza utendaji wa Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika wizara mbali mbali katika kuwatumikia wananchi. Mwakilishi wa Kojani, Hassan Hamad Omar, alipopata nafasi ya kuuliza swali na kutaka kujua mikakati ya kuimarisha huduma katika wilaya ndogo ya kisiwa cha Kojani Pemba, alisema mawaziri wa Serikali ya Zanzibar wameonyesha kasi nzuri ya utendaji ambayo imejikita katika kuwatumikia wananchi kupata huduma bora.

''Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa mawaziri wetu wa serikali kwa mwanzo mzuri na kuchapa kazi kwa ajili ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar,'' alisema.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara ya Maalumu za SMZ, Masoud Ali Mohamed, alisema katika kuimarisha huduma katika wilaya ndogo za kisiwa cha Kojani, serikali ipo katika hatua za mwisho za kufungua ofisi ndogo ya usajili wa matukio ya kijamii ikiwamo vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi.

Alisema lengo la kufikisha huduma hizo karibu na wananchi ni kuwapunguzia usumbufu kufikisha huduma zote za kijamii ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kutekeleza mpango wa ugatuzi.

''Mheshimiwa Spika, napenda kumjulisha Mwakilishi wa Jimbo la Kojani kwamba huduma muhimu ikiwamo za usajili wa vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi zitafikishwa katika kisiwa cha Kojani haraka,'' alisema.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiwa na baadhi ya wahariri na waandishi wa habari wa vyombo mbalimbali, baada ya kumaliza mkutano wake na vyombo hivyo, Ikulu jijini Zanzibar juzi. **PICHA: IKULU**

# Mchakato usajili wa madrasa waanza

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema imeanza mchakato wa kusajili madrasa kwa ajili ya kudhibiti na kuweka utaratibu mzuri wa kutoa elimu ya dini kupitia madrasa hizo.

Hayo yalisemwa jana katika Baraza la Wawakilishi jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora), Haroun Ali Suleiman, wakati akijibu suali la Mwakilishi wa kuteuliwa na rais, Sada Mkuya Salum, aliyetaka kujuwa lini Serikali itaanza usajili wa madrasa.

Alisema Serikali imeanzisha utaratibu huo kwa ajili ya kuzitambua na kuweka utaratibu mzuri wa kuendesha shughuli zao za kutoa elimu kwa wanafunzi.

Alieleza jumla ya madrasa 1,011 zimesajiliwa na kutambuliwa kwa upande wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja na Mkoa wa kaskazini Unguja.

Aidha alisema usajili wa madrasa unakwenda sambamba na usajili wa misikiti katika Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja ambapo misikiti 817 imetambuliwa.

''Mheshimiwa Spika, napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba tumeanza mchakato wa kusajili madrasa zinazotoa elimu ya Quran ambapo kazi hiyo imeanza kwa upande wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja na Kaskazini Unguja...tunaendelea na kazi hiyo.' 'alisema Waziri huyo.

Aalisema wizara ipo katika hatua za mwisho za kutayarisha mitaala ya masomo ambayo itatumika kwa walimu wote wa madrasa Unguja na Pemba.

Alisema mchakato huo ni muhimu ambao utakawenda sambamba na usajili wa walimu hao kwa kuwafanyiwa mahojiano ili kuwapata wenye sifa za kutoa huduma za elimu kwa wanafunzi na kuepukana na matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

# Risiti za kimtandao kwa w/biashara Aprili

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Jamal Kassim Ali, amesema mfumo wa kutoa risiti kielektroniki kwa wafanyabiashara unatarajiwa kuanza rasmi kazi Aprili, mwaka huu.

Waziri huyo amesema lengo ni kukusanya kodi na kudhibiti mianya ambayo huikosesha Serikali mapato.

Aliyasema hayo jana wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Mfenesini, Machano Othman Said, aliyetaka kujua lini Serikali itaanzisha mfumo wa kutoa risiti kwa njia ya kielektroniki na kudhibiti mapato.

Kassim alisema awali Serikali ilianzisha huduma za kutoa risiti kwa njia ya kielektroniki kwa wafanyabiashara 150 kama majaribio, lakini zoezi hilo lilisita baada ya kubainika kujitokeza kwa kasoro za kiufundi kwa mashine hizo.

''Mheshimiwa Spika, napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba Serikali inatarajia kuanza kutoa risiti kwa njia ya kielektroniki kuanzia Aprili mwaka huu,'' alisema.

Alisema kukosekana kwa mashine za kielektroniki kwa wafanyabiashara kwa kiasi kikubwa hulikosesha taifa fedha nyingi ambazo zingetumika kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi.

Aidha Waziri huyo aliwataka wafanyabiashara na vituo vya kutoa huduma za mafuta kuhakikisha wanatoa risiti wanapotoa huduma kwa wananchi.

Alisema sheria ya usimamizi wa kodi namba saba ya mwaka 2019 imeweka inaelekeza wafanyabiashara wote kutoa risiti wanapotoa huduma za kibiashara.

Alieleza kitendo cha wafanyabiashara kukataa kutoa risiti wanapotoa huduma ni kosa, na watakaobainika watachukuliwa hatua za kisheria.

''Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi ya kuwataka wafanyabiashara katika vituo vya kutoa huduma za mafuta kutoa risiti baada ya kufanya manunuzi......kitendo cha kukataa kutoa risiti ni kosa kwa mujibu wa sheria za usimamizi wa kodi,'' alisema.

**''Mheshimiwa Spika, napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba Serikali inatarajia kuanza kutoa risiti kwa njia ya kielektroniki kuanzia Aprili mwaka huu,'' alisema.**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SAID ALI KARUME** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA PRADO** yenye namba za usajili **T 992 AYT chasisi namba RZJ950029576** engine namba **3RZ215848** ,yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **Polisi taarifa KAWE/RB/250/2021**

## KUPOTEA KWA CHETI



**AGOSTINO ISOMBA** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S665/030** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya Secondary **MWEMBENI-MUSOMA** mwaka 1993,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa DAR/MAG/RB/78934/2021**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**FORM II**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**ARUSHA MJINI**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 38/2021**

Ombi la **LUCY F. MSANGI** na **CHRISTOPHER F. MSANGI** kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **FREEDOM HEZEKIA MSANGI**

Kwa **YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII POPOTE ALIPO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo **tarehe 23/02/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo. Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 9/2/2021.**

MASE INTERNATIONAL LTD

## NOTISI / TANGAZO LA MNADA WA HADHARA –MWANZA

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA EQUITY BANK(TANZANIA)LIMITED – MAKAO MAKUU DAR ES SALAAM, TUNAKUTAKA MTEJA TULIE KUTAJA KATIKA JEDWARI CHINI ULIPE DENI LAKO LOTE NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14) KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI, ENDAPO UTASHINDWA/UTAKAIDI AGIZO HILI BASI MALI ZAKO ULIZOWEKA KAMA DHAMANA YA MKOPO ZITAUZWA KWA MNADA WA HADHARA KAMA ZILIVYO ORODHESHWA KWENYE JEDWALI CHINI

| S/NO. | JINA LA MDAIWA | JINA LA MMILIKI WA DHAMANA | DHAMANA | MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA NA MUDA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | RASHID MADUHU KABESI | RASHIDI MADUHU KABESI | 1.NYUMBA, PLOT NO.933,BLOCK"A"<br>2.NYUMBA,PLOT NO.931,BLOCK"A" | 1.MHANDU-MWANZA<br>2.MHANDU-MWANZA | 26/02/2021 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA<br>26/02/2021 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**
1. UKAGUZI WA DHAMANA NI KWA KUWASILIANA NA DALALI.
2. MNUNUZI ATALIPA ASILIMIA 25% YA BEI ILIYOFIKA SIKU YA MNADA NA SALIO LA ASILIMIA 75% ATALIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE TOKEA SIKU YA MNADA, NA ENDAPO MNUNUZI ATASHINDWA KUMALIZIA SALIO LA ASILIMIA 75% NDANI YA SIKU KUMI NA NNE BASI MNUNUZI ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI ZAKE ZOTE NA PESA ALIZOLIPA AWALI HATA RUDISHIWA NA DHAMANA ITAUZWA UPYA.
3. GHARAMA ZA KUBADILI UMILIKI NI ZA MNUNUZI, KUMBUKA VIGEZO NA MASHARTI KUZINGATIWA.
4. GHARAMA ZA KUMTOA MDAIWA (MWENYE NYUMBA AU WAPANGAJI) NI ZA MNUNUZI WOTE MNAKARIBISHWA

**MKURUGENZI MTENDAJI**
**EQUITY BANK(TANZNIA)LIMITED**
**MASE INTERNATIONAL LTD**
**P.O.BOX 11083 DAR ES SALAAM**
**P.O.BOX 6197 MWANZA**
**SIMU: 0742819940 SIMU: 0710885084**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ANNA ISAAC ZUMBA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.174 CHY** AINA **TOYOTA ALLEX** RANGI NYEUSI. **CHASSIS NAMBA NZE1210231924.ENGINE INZSE1496ML.**YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.**TAARIFA YA POLISI MBE/MBE/RB/477904/2021.**

K-FINANCE
Financing. Advisory. Training

## NOTISI

Kampuni ya **K-FINANCE** inatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kwa mdaiwa (Mkopaji) **CLOUD KAIGARULA CHRISTOPHER** na mdhamini wake **NTEZIMA BELEGELE** wanatakiwa kulipa deni lote ndani ya muda uliotolewa. Ikiwa watashindwa kulipa ndani ya muda tajwa, dhamana ambayo ni Gari litauzwa kwa mnada wa hadhara.

Judith Minzi
Mkurugenzi Mtendaji
K-finance Limited

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na 0738165606 na 0738165605.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO...... OF 2021**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE GLORIA DAVID MUBEYA**
And
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY NOEL MUBEYA**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before **24 Day of February 2021**
Dated at Dodoma this **4TH Day of February 2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MAJID ABDALLAH MASSARE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI FUSO** yenye namba za usajili **T 935 ALG,** Yenye chassis namba **FK4171551512 na Engine namba 6D17756202.**
Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **Taarifa ya polisi: MOS/TR/RB/242/2021.**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 1 OF 2021**

In the Matter of the Estate of the Late **DENIS LWEUMBIZA RWEKAZA BY LETICIA KOKUBANZA ALOYCE** all persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the Proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of Administration) is made to the above-named petitioner
Objection to the grant should be field on or before the 15 day of March 2021
Dated at Morogoro this 10 day of February 2021.

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**




OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Waandamana kupinga gharama maisha kupanda

**Khartoum, SUDAN**

MAANDAMANO mapya dhidi ya kupanda kwa gharama ya maisha yamefanyika Jumanne wiki hii, nchini Sudan, baada ya shida za kiuchumi.

Nchi hiyo yenye watu milioni 40, kwa siku moja imekumbwa na maandamano hayo baada ya kuundwa kwa serikali mpya.

Serikali mpya, ina jukumu la kuiondoa nchi hiyo kwenye mgogoro wa kiuchumi, uliodumu miongo kadhaa na baada ya kuanguka utawala wa Omar Al-Bashir.

Al-Bashir, alitimuliwa na jeshi chini ya shinikizo kutoka mitaani mwezi Aprili 2019.

Wiki za hivi karibuni, maandamano dhidi ya gharama kubwa ya maisha yameongezeka, hasa katika mji mkuu Khartoum na katika Jimbo la Gedaref, Mashariki.

Kutokana na uhaba wa bidhaa mbalimbali, raia wa Sudan wanalazimika kusubiri saa nyingi kwenye foleni mbele ya vituo vya mafuta, maduka ikiwamo ya dawa.

"Hatutaki bei ya juu, hatutaki kufa na njaa," waandamanaji walisema huko Nyala, Mji Mkuu wa Jimbo la Darfur Kusini Magharibi.

Huku wakichoma moto maduka na kurusha mawe kwa polisi, walitawanywa wakitumia gesi ya machozi, lilibainisha Shirika la Habari la AFP.

Waziri Mkuu, Abdallah Hamdok, wiki hii, alisema serikali yake mpya itatoa kipaumbele kwa uchumi pia alizungumza kwa njia ya simu na Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, ambaye alielezea kuunga mkono serikali ya mpito.

Wawili hao walijadili njia za kukuza maendeleo na mageuzi ya kiuchumi, kwa kutekeleza makubaliano ya amani ya hivi karibuni na kushughulikia chanzo cha vurugu huko Darfur.

Mwaka jana, Washington, iliiondoa Khartoum kwenye orodha ya nchi ambazo Marekani inazituhumu kufadhili ugaidi.

*RFI*




Watawa wa Kibuddha wakiongoza maandamano kupinga mapinduzi ya kijeshi nchini Myanmar, jana, katika mkoa wa Mandalay. Jeshi la nchi hiyo limepiga marufuku maandamano ya umma katika miji miwili mikubwa nchini humo. **PICHA/AP**

# Makao makuu ya chama Suu Kyi yavamiwa na jeshi

**Nay Pyi Taw, MYANMAR**

WANAJESHI wamevamia na kuharibu ofisi za makao makuu ya Chama cha National League of Democracy (NLD) cha Aung San Suu Kyi, chama hicho kimesema.

BBC Burma, ilisema inafahamu kuwa vikosi vya usalama vimevunja milango kwa nguvu majira ya jioni Jumanne.

Hakuna wanachama wa chama waliokuwapo katika jengo hilo wakati huo.

Shambulio hilo linakuja wakati maelfu wakiendelea kupinga mapinduzi ya kijeshi ambayo yalikiondoa NLD kutoka serikalini.

Wengi wanadai kuachiliwa kwa Suu Kyi na washirika wakuu wa NLD, ambao hawajulikani walipo.

"Dikteta wa kijeshi alivamia na kuharibu makao makuu ya NLD karibu saa 9:30 alasiri," NLD ilitangaza kwenye ukurasa wake wa Facebook na haikutoa maelezo zaidi.

Uvamizi huo ulifanyika wakati wa amri ya kutotoka nje ya nchi nzima usiku, ambayo huanza saa mbili usiku hadi saa 10 alfajiri. Mikusanyiko ya zaidi ya watu watano pia imepigwa marufuku.

Waandamanaji wanaingia barabarani kwa siku ya tano mfululizo na polisi kujibu kwa matumizi makubwa ya nguvu na kusababisha majeruhi kadhaa yaliyoripotiwa. Jana, kundi la watumishi wa umma lilikusanyika katika mji wa Nay Pyo Taw, liliripoti gazeti la Myanmar Now.

Wanajeshi walichukua udhibiti Februari Mosi, mwaka huu, baada ya uchaguzi mkuu ambao Suu Kyi wa Chama cha NLD, kikishinda kwa kishindo.

Vikosi vya wanajeshi viliunga mkono upinzani, waliodai marudio ya kura, wakidai udanganyifu ulifanyika.

Tume ya uchaguzi ilisema hakuna ushahidi wa kuunga mkono madai hayo.

Suu Kyi yuko chini ya kizuizi cha nyumbani na maofisa wengine, jeshi likisema litafanya uchaguzi huru na wa haki, hali ya hatari ikiisha.

*BBC*

## Uganda yaondoa vizuizi mitandao ya kijamii

**Kampala, UGANDA**

SERIKALI ya Uganda, imetangaza kuondoa vizuizi vyote ilivyokuwa imeviweka katika intaneti na mitandao ya kijamii.

"Tunaomba radhi kwa usumbufu wowote uliojitokeza, lakini ilikuwa ni kwa ajili ya usalama wa taifa letu," Peter Ogwang, Waziri wa Mawasiliano, aliandika kwenye tweeter.

Aliongeza: "Tuwe wateja wa kujenga na sio kubomoa, tuwe wateja wazuri wa mitandao ya kijamii."

Huduma ya mitandao ya kijamii ilizuiwa usiku wa kuamkia Januari 14, mwaka huu, siku ya uchaguzi mkuu.

Rais Yoweri Museveni alishutumu kampeni za mitandao ya kijamii kuwa na ubaguzi.

Hatua hiyo ilikuja baada ya Facebook kusema kuwa inazifungia zaidi ya akaunti 200 zinazohusiana na kampeni za chama tawala.

Kampuni ya mitandao ya kijamii, ilidai kuwa akaunti hizo zilikuwa zinasambaza taarifa zisizo sahihi kudhibiti mijadala kabla ya siku ya kupiga kura.

Facebook ilisema akaunti hizo zilikuwa za Uganda, na zilituma taarifa za kughushi kwa wananchi na kutuma taarifa hizo ili kuzipa umaarufu zaidi.

Mkuu wa Taarifa za Vitisho Facebook, David Agranovich, alisema uchunguzi wao ulibaini kuwa unahusisha akaunti feki zilizohusisha moja kwa moja wizara ya mawasiliano na teknolojia.

Facebook pia iliondoa akaunti 139 za Instagram.

Akaunti hizo zilikuwa zinamuunga mkono Rais Museveni na chama chake cha National Resistance Movement (NRM).

Mpinzani wake mkuu ambaye ni mwanamuziki aliyegeuka kuwa mwanasiasa, Robert Kyagulanyi maarufu Bobi Wine, alikuwa na miaka minne, wakati wakati Museveni akiingia madarakani, mwaka 1986.

*BBC*

## Kesi dhidi ya Trump yaanza kusikilizwa

**Washington, MAREKANI**

BARAZA la Seneti, jana, limeanza kusikiliza kesi iliyowasilishwa dhidi ya Trump.

Kesi ya Donald Trump, ambaye alishtakiwa kwa uchochezi wa uasi katika uvamizi wa bunge Januari 6, mwaka huu, nchini Marekani, anatuhumiwa kwa mara ya pili katika historia ya nchi.

Trump, alishtakiwa katika Baraza la Wawakilishi kama sehemu ya uchunguzi wa Ukraine, mwishoni mwa mwaka 2019.

Aliachiliwa huru kwa kura za maseneta wa Chama cha Republicans katika Seneti, Februari, mwaka jana.

Mkutano Mkuu wa Seneti utaamua iwapo Trump ana hatia kusababisha uvamizi wa bunge na umwagaji damu uliopelekea vifo vya watu watano na uchochezi baada ya mchakato wa kura katika Baraza la Wawakilishi, Januari 14, mwaka huu.

Hivyo basi, Trump atarekodiwa kama rais wa kwanza kuhukumiwa kwa mara ya pili katika historia ya Marekani, na rais pekee ambaye alishtakiwa kwa ombi la kufutwa kazi baada ya kipindi chake cha utawala kumalizika.

*TRT*




# SALIBA:

## ARTETA HAKUTAKA KUNIPA MUDA ARSENAL

**NICE, Ufaransa**

WILLIAM Saliba amehoji juu ya uamuzi wa haraka uliyofanywa na Mikel Arteta dhidi yake katika timu ya Arsenal, huku beki huyo mwenye kiwango cha juu akidai kuwa alipewa "mechi mbili na nusu" zisizo na ushindani ambazo ni ngumu kuthibitisha ubora wake.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, alijiunga na 'Washikabunduki' hao wakati wa msimu wa joto wa 2020, miezi 12 kutoka Saint-Etienne.

Wakati akisubiri kupata nafasi ya kucheza Arsenal, Arteta alimpeleka kwa mkopo kule Nice.

"Arteta alinihukumu kwa mechi mbili na nusu," alisema Saliba akiiambia RMC Sport.

"Ningependa anichezeshe zaidi. Lakini aliniambia sikuwa tayari.

"Nilikuwa nikimsubiri anipe nafasi, lakini mambo ya soka kama unavyojua.

"Ninajua kuwa wakati mwingine ni ngumu kuelezea au kuelewa baada ya fedha ambazo klabu ilitumia kunitoa, kunipeleka kwa mkopo, lakini mambo mengi yamenitokea."

Arsenal iliwekeza pauni milioni 27 kwa Saliba wakati ilipomnunua kutoka Saint-Etienne.




## SUAREZ AJIWEKEA REKODI YAKE LALIGA

**MADRID, Hispania**

LUIS Suarez ameweka rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza kwenye historia ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kufunga mabao 16 katika mechi 17 za mwanzo akiwa na timu mpya.

Suarez alitemwa na Barcelona na akajiunga na Atletico Madrid kuelekea kuanza kwa msimu huu.

Suarez amekuwa mchezaji muhimu kwenye kikosi cha kocha Diego Simeone msimu huu kwa uhodari wake wa kuzifumania nyavu, ni kitu kinachomfanya mchezaji huyu kuwa na nafasi ya kipekee kwenye kikosi cha Atletico.

Katika mchezo dhidi ya Celta Vigo usiku wa kuamkia jana, Suarez alipachika mabao mawili katika mchezo ulimalizika kwa sare ya 2-2 na kuendelea kujiimarisha katika nafasi ya kwanza kwenye msimamo wa LaLiga msimu huu.

Mabao hayo yakamfanya Suarez kuwake rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza kwenye historia ya LaLiga kufunga mabao 16 katika michezo 17 ya mwanzo akiwa na timu mpya.

Cristiano Ronaldo aliweka rekodi hiyo kwa kupachika mabao 15 alipotua Real Madrid akitokea Manchester United mwaka 2009.

Kwa hali ilivyo kwa sasa, Suarez anaongoza kwa kupachika mabao 16 akimzidi Lionel Messi (13) katika orodha ya wafungaji kwenye LaLiga msimu huu.

## AGUERO NI MUDA TU KUREJEA - GUARDIOLA

**MANCHESTER, England**

SERGIO Aguero amepata ahueni, lakini hatakuwa tayari kurudi uwanjani haraka, kwa mujibu wa kocha wake, Pe Guardiola.

Mshambuliaji huyo wa Manchester City alirudi mazoezini wiki hii na ameanza kufanya kazi na kikosi cha kwanza baada ya kupona virusi vya corona.

Lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, hajacheza mechi tangu Oktoba mwaka jana na anahitaji kupata afya nzuri kabla ya kurejea uwanjani.

"Juzi, alifanya mazoezi ya dakika 10 hadi 15 na kundi la wachezaji wenzake na baadaye kufanya mazoezi peke yake," alisema Guardiola katika mkutano wake na waandishi wa habari. "Siku baada ya siku anajisikia vizuri."

Alipoulizwa ikiwa alikuwa tayari kurudi, aliongeza: "Bado."

Wakati wa kucheza bila washambuliaji, Guardiola alisema: "Tusipocheza na beki wa kati wa kawaida watu wanaweza kusonga mbele zaidi, lakini tunapaswa kufika kwenye sanduku.

"Tuliona kwenye mchezo dhidi ya Liverpool, wachezaji wanne au watano walikuwa ndani ya sanduku. Kila mchezo ni tofauti. Alikuwa tayari kuanza mechi ya raundi ya tatu ya Kombe la FA dhidi ya Birmingham City, lakini alilazimika kujitenga baada ya kuwasiliana kwa karibu na mtu ambaye alikuwa ameambukizwa corona.



# HABARI MICHEZO

UZINDUZI...



Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Airtel Tanzania, Beatrice Singano (kushoto), akizungumza jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa Airtel TV, inayolenga kukuza mtindo wa maisha ya kidigitali na kuongeza upatikanaji wa maudhui ya ndani nchini. Katikati ni Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Filamu Tanzania, Dk. Kiagho Kilonzo na Rais wa Shirikisho la Wasanii wa Filamu Tanzania, Elia Mjata. **MPIGAPICHA WETU**

# Airtel yazindua Airtel TV App kuinua kazi za wasanii nchini

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Airtel Tanzania, imezindua rasmi Airtel TV ikiwa na lengo la kukuza na kuendeleza huduma zake bora za kidigitali na kuongeza kasi ya usambazaji wa kazi za sanaa za wasanii wa hapa nchini.

Kazi hizo za wasanii wa hapa nchini sasa zitaonekana sasa na kupatikana moja kwa moja kupitia Televisheni Mtandao ya Airtel ijulikanayo kama Airtel TV App, na kuwapatia wateja wa Airtel burudani zaidi wakiwa popote hapa nchini.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Televisheni Mtandao ya Airtel, Kaimu Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu Tanzania, Dk. Kiagho Kilonzo, alisema uzinduzi wa Televisheni Mtandao ya Airtel (Airtel App) ni ushuhuda kwamba tasnia ya sanaa na burudani nchini hususan filamu za Kitanzania (Bongo movies) inakua na inaweza kupatikana kupitia majukwaa tofauti.

Alisema Televisheni Mtandao ya Airtel itakuwa na programu mbalimbali kama vile sinema, tamthilia, maandishi, muziki na katuni, na zote zitakuwa zikijumuisha kazi zilizozalishwa nchini na wasanii wa hapa pamoja na za kimataifa.

"Leo hii nachukua fursa kuipongeza Kampuni ya Airtel kwa kuzindua Televisheni Mtandao, kwa kuwa wasanii wetu watakuwa na jukwaa la kidigitali la kuonyesha kazi zao na kwa hivyo si tu kuongeza ufikishaji wa kazi zao kwa mashabiki wengi, bali pia itawaongezea mapato.

"Natoa wito kwa wasanii wetu kote nchini, kuchangamkia fursa hii kwa kuendelea kutengeneza kazi nyingi zenye viwango zaidi, kwani Televisheni Mtandao (Airtel App) itawaongezea umaarufu, mashabiki pamoja na watazamaji wengi nchini na hata nje ya Tanzania," alisema.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Airtel, Beatrice Singano, alisema Airtel imejitolea kuendelea kuleta huduma hii yakibunifu nchini Tanzania ili kukidhi mahitaji ya wateja wa Airtel na kundelea kufurahia kuwa ndani ya mtandao bora wa Smartphone na kuishi kidigitali.

"'Aplikesheni' hii mpya ya Airtel TV App itawawezesha wateja kupata habari za uhakika, sinema, muziki, vipindi vya tamthilia, vipindi vya watoto pamoja na maandishi. Maudhui na kazi hizi zote ndani ya Airtel TV App zitatoka ulimwenguni kote ikiwa ni pamoja na Hollywood, Bollywood, na Nollywood na kwa zaidi sinema zetu za Bongo.

"Tunayo furaha kubwa kuwaletea jukwaa la kisasa ambalo litakutanisha wapenda burudani na filamu wazipendazo. Na tunaamini idadi itakuwa ikiongezeka katika kipindi cha kila mwaka, pale tunapoongeza maudhui ya kuelimisha wateja wetu wote," alisema Singano.

Naye Rais wa Shirikisho la Wasanii wa Filamu Tanzania, Elia Mjata, aliipongeza Airtel kwa kuja na applikesheni ya Airtel TV - ambayo itaipa tasnia hiyo jukwaa la kuonyesha vipaji vya wasanii wa Tanzania kupitia simu za mkononi na vilevile kuzipaisha kazi zao nje ya mipaka ya Tanzania.

BONASI...




Mshindi wa mechi 11 za Jackpot Bonus, Saidy Shabani, akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 7.5 baada ya kukabidhiwa na Kampuni ya SportPesa. Jackpot kwa wiki hii ni shilingi 456,673,160 kwa atakayepatia mechi zote 13, huku watakaobashiri kwa usahihi kuanzia mechi 10-12 wakipata bonasi. **PICHA: SPORT-**

# Yanga sasa yaelekeza nguvu zaidi Kombe la FA

**Na Saada Akida**

MKURUGENZI wa mashindano wa Yanga, Thabit Kandoro, amesema kulingana na mipango waliojiwekea msimu huu, ana imani na timu yao kuwa hakuna timu ambayo itawazuia kufikia malengo ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA.

Kandoro aliliambia gazeti hili baada ya kumaliza vizuri mzunguko wa kwanza na kuweka rekodi ya kutopoteza mechi, sasa wamejipanga kikamilifu kuhakikisha wanaendelea pale 'walipoishia'.

Alisema baada ya uongozi kuweka mipango vizuri ikiwamo mazingira bora na kulipa mishahara ya wachezaji kwa wakati, wanaamini watapambana na kujitoa kutafuta ushindi kwa kila mechi watakayocheza.

"Nina imani kwenye Ligi kila kitu kinaenda vizuri, tumejipanga kuhakikisha timu inapata mahitaji yote, huku benchi la ufundi likiwa limekamilisha mapendekezo yao ya usajili kazi iliyobaki ni kwenda kupambana kutafuta matokeo chanya uwanjani," alisema Kandoro.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, alisema ameanza kufanyia kazi upungufu wao ikiwamo utulivu na umakini wa safu ya ushambuliaji ambayo ni muhimu katika kufanikisha ushindi.

"Hatuwezi kupata ushindi bila kufunga, tunatakiwa kuwa makini hasa katika nafasi tunazotengeneza kuhakikisha tunafunga mabao ili kuendelea kujiimarisha zaidi na kuendelea kubaki hapa juu tulipo, tunatakiwa kupambana na kila timu bila kujali nafasi na jina la mpinzani ambaye tunakutana naye," alisema Kaze.

Tayari Yanga ambayo inaongoza msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 44, ipo jijini Mbeya ikijiandaa na mechi ya ligi hiyo itakayopigwa keshokutwa, Jumamosi dhidi ya Mbeya City katika Uwanja wa Sokoine.

Mabingwa watetezi Simba ambao wapo nyuma mechi moja, wanashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo wakiwa na pointi 39 wakifuatiwa na Azam yenye alama 33 ikiwa imecheza mechi 18 sawa na Yanga iliyopo kileleni.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BENZEMA: MBIO UBINGWA REAL MADRID BADO NGUMU

Kila mchezo ni fainali na tunatakiwa kushinda kila mmoja, tunajiamini kwani mara zote...

**MADRID, Hispania**

KARIM Benzema amesisitiza "kuna safari ndefu ya kwenda" kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, baada ya Real Madrid kupunguza gepu na vinara Atletico Madrid.

Benzema alifunga bao la ufunguzi na Ferland Mendy akaongeza la pili kukiwezesha kikosi hicho cha kocha, Zinedine Zidane kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Getafe, Jumanne.

Atletico walitoka sare ya 2-2 nyumbani na Celta Vigo Jumatano wakati Los Blancos wakipunguza gepu la pointi hadi tano pale kwenye dimba la Alfredo Di Stefano, ingawa kikosi cha Diego Simeone bado kina mechi mbili mkononi.

Lakini hilo halimsumbui Benzema, ambaye alifunga bao hilo kwa kuunganisha krosi ya Vinicius Junior likiwa ni la 16 msimu huu kwenye mashindano yote, na mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa anaamini Madrid wapo kwenye njia moja na Atletico.

"Lilikuwa bao zuri, pasi nzuri kutoka kwa Vini na mpira ukaingia ndani moja kwa moja. Nafikiri tulikuwa tumerudi vizuri," alisema Benzema akiiambia Movistar.

"Mara zote ni mchezo mgumu dhidi ya Getafe. Tutaendelea kucheza kama hivi. Kuna safari ndefu ya kwenda hadi mwisho.

"Kila mchezo ni fainali na tunatakiwa kushinda kila mmoja. Tunajiamini.

"Mara zote kuna kelele nyingi pale Madrid kwa sababu hii klabu ni bora duniani."

Mchezo unaofuata wa Madrid ni dhidi ya Valencia Jumapili, wakati vinara wa msimamo, Atletico watacheza na Granada Jumamosi.

Wanaoshika nafasi ya pili, Barcelona, ambao wamepitwa pointi tatu na Madrid na pointi nane na vinara, watacheza na Deportivo Alaves Jumamosi.

## KWA UFUPI

**MIAMI KWA GIBBS, SHAWCROSS**

KLABU ya Inter Miami, inayoshiriki Ligi Kuu Marekani (MLS), inayomilikiwa na David Beckham chini ya kocha, Phil Neville, inataka kuwasajili wachezaji wa zamani wa England, Ryan Shawcross mwenye umri wa miaka 33, kutoka Stoke City na mlinzi wa pembeni, Kieran Gibbs, 31, kutoka West Brom. ***(Sun)***

**CITY KUACHANA NA MARTINEZ**

MANCHESTER City inataka kuachana na mpango wake wa kutaka kumsajili mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez, wakati nyota huyo mwenye umri wa miaka 23 akitarajia kusaini mkataba mpya na miamba hao wa Serie A. ***(Eurosport)***

**SOLSKAJAER KUPEWA MKATABA**

MANCHESTER United itasubiri hadi mwishoni mwa msimu huu kabla ya kufungua mazungumzo ya mkataba mpya na kocha wake, Ole Gunnar Solskjaer, ambaye huu wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu wa 2021-22. ***(Sun)***

**MADRID YAJIPANGA KWA ALABA**

REAL Madrid inapanga kumsajili mlinzi wa kushoto wa Bayern Munich na Austria, David Alaba mwenye umri wa miaka 28, huku Chelsea ikishindwa kufikia mshahara anaoutaka mlinzi huyo wa pauni 400,000 kwa wiki. ***(ESPN)***

**MILAN NA IBRAHIMOVIC**

AC Milan inapanga kufungua mazungumzo na straika wa Sweden, Zlatan Ibrahimovic mwenye umri wa miaka 39, kuhusu mkataba mpya utakaomweka hapo hadi akiwa na umri wa miaka 41. ***(Sun)***

**STONES KUPEWA MKATABA**

MANCHESTER City itafungua mazungumzo ya mkataba mpya na John Stones mwenye umri wa miaka 26, kipindi cha majira ya joto, kutokana na kiwango alichokionyesha mlinzi huyo. ***(Times)***

**HODGSON NA HATIMA YAKE**

KLABU ya Crystal Palace haina uhakika kama itampa mkataba mpya kocha wake, Roy Hodgson mwenye umri wa miaka 73, msimu ujao. Mkataba wa sasa wa kocha huyo wa zamani wa England unamalizika kipindi cha majira ya joto. ***(Mail)***

**GAYLE KUONDOKA NEWCASTLE**

STRAIKA wa Newcastle United, Dwight Gayle mwenye umri wa miaka 31, amechukizwa na kukosa muda wa kucheza pale St James' Park na anaweza kuondoka akiwa mchezaji huru mara mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Chronicle)***

**OLSEA ATAKA MKATABA**

GOLIKIPA wa Sweden, Robin Olsen mwenye umri wa miaka 31, anataka kubadilishwa kwa uhamisho wake wa mkopo kutoka Roma kwenda Everton na kuwa wa kudumu. ***(Goal)***

**EDERSON KUPIGA PENALTI**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, anataka kumkabidhi golikia, Ederson mwenye umri wa miaka 27 jukumu la kupiga penalti - baada ya timu hiyo kukosa tatu kati ya saba walizopata msimu huu. ***(Independent)***

**NEVILLE ATAKA MAN KUSAJILI BEKI**

MLINZI wa zamani wa Manchester United, Gary Neville, amesema klabu yake hiyo ya zamani inapaswa kusajili mlinzi wa kati kipindi cha majira ya joto. ***(Sky Sports, via Goal)***

## HABARI MICHEZO

# CHAMA AONGOZA KWA 'ASISTI' LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Simba, Mzambia Clatous Chama, anaongoza kwa kutoa pasi za mwisho 'asisti' zilizozaa mabao kwenye timu yake mpaka sasa katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu unaoendelea.

Kwa mujibu wa takwimu za Ligi Kuu Tanzania Bara, Chama ametoa pasi za mwisho nyingi zaidi kwenye ligi hiyo kuliko mchezaji mwingine yeyote, akifuatiwa na winga Luis Miquissone kutoka Msumbiji, ambaye naye ni wa Simba.

Mpaka sasa Chama ana asisti tisa, huku mwenyewe akiwa amepachika mabao sita kwenye nyavu.

Wakati Chama akiwa anaongoza kwa watoa pasi za mwisho, Miquissone anafuatia akiwa ametoa asisti nane, akizidiwa moja tu na Chama, lakini yeye akifunga mabao mawili tu, akizidiwa manne na mwamba huyo wa Lusaka.

Mchezaji anayeshika nafasi ya tatu kwa 'asisti' ni Rajab Athumani wa Gwambina ya jijini Mwanza ambaye ana asisti sita, lakini akiwa hajafunga bao lolote, na nafasi ya nne inashikiliwa na straika wa Azam FC, Prince Dube.

Mpaka sasa straika huyo, mbali na kupachika mabao sita kwenye nyavu, lakini ametoa asisti tano mpaka sasa , huku beki David Luhende wa Kagera Sugar naye akiwa na 'asisti' tano, lakini akifunga bao moja tu mpaka sasa.

Straika wa Yanga, Yacouba Songne naye yumo kwenye orodha ya kumi bora ya wapiga pasi za mwisho kwenye Ligi Kuu Bara, baada ya kuwa na asisti nne, huku mwenyewe akitupia mara nne pia, kiungo wa Azam FC, Idd Nado naye pia akiwa na 'asisti' nne na mabao manne.

Abdurahman Mussa, straika wa Ruvu Shooting, naye pia ana asisti nne kama Songne na Nado, lakini yeye amefunga mabao mawili tu.




Meneja Masoko wa Kampuni ya M-Bet Tanzania, Allen Mushi (kulia), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 85.9 kwa Dominic Mdimi (kushoto) na Valentino Ngolle, baada ya kufanikiwa kubashiriki kwa usahihi mechi 12 za ligi mbalimbali duniani. Washindi hao pia ni mashabiki wa Yanga. **MPIGAPICHA WETU**

# Mashabiki Yanga kicheko na M-Bet

**Na Mwandishi Wetu**

MASHABIKI wawili wa timu ya Yanga wameibuka washindi wa Sh. milioni 85.9 baada ya kubashiri kwa usahihi jumla ya michezo 12 ya mchezo wa kubahatisha wa Perfect 12 wa Kampuni ya M-Bet Tanzania.

Meneja Masoko wa M-Bet Tanzania, Allen Mushi, aliwataja washindi hao ni Dominic Mdimi ambaye ni shabiki wa Yanga ambapo amefanikiwa kushinda kwa mara ya pili droo ya Perfect 12. Mdimi alishinda zawadi nyingine ya Sh. milioni 36, Oktoba mwaka juzi.

Mushi alimtaja mshindi mwingine ni Valentino Ngole wa Njombe ambaye pia ni shabiki wa Yanga ameshinda kwa mara ya kwanza katika droo hiyo.

Alisema kuwa Mdimi na Valentino wanakuwa washindi wa saba tangu kuanza kwa mwaka huu na kuendelea kuinua vipato vya Watanzania.

Kwa upande wa Mdimi alisema kuwa ushindi wake umetokana na kuwa makini katika kuchagua timu bila ya kufuata alama za ushindi ambazo kila timu imekuwa ikipewa katika mkeka.

Alisema pamoja na ushindi huo bado timu ya Arsenal inampa changamoto sana, hata hivyo, safari hii haikuwapo katika mkeka ambao yeye alibashiri.

Ngolle alisema amefarijika sana na ushindi huu kwani utamfanya kufungua biashara ili kujiongezea kipato.

"Nilikuwa nabashiri na kupata fedha kidogo kama Sh. 200,000 na fedha nyingine kidogo, sijakata tamaa na sasa kufanikiwa kupata fedha ambazo nitafanyia masuala ya maendeleo," alisema Ngolle.

## Badru sasa kocha mkuu Gwambina

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Gwambina FC, umeingia makubaliano na aliyekuwa Kocha wa Malindi ya Zanzibar, Mohamed Badru Juma, kuwa Kocha Mkuu wa timu hiyo akichukuwa nafasi ya Novatus Fulgence.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Gwambina FC, Daniel Kilai, alisema wameingia mkataba wa mwaka mmoja na Badru baada ya kupitia wasifu [CV] za makocha wengi wazawa na uongozi kuridhishwa na kocha huyo.

Alisema tayari kocha huyo ameanza kazi rasmi tangu mwanzoni mwa wiki hii na leo atakuwapo kwenye benchi la ufundi wakati timu hiyo ikicheza dhidi ya Kagera Sugar.

"Tulipokea maombi mengi kutoka nje na ndani ya Tanzania, malengo yalikuwa kutafuta kocha mzawa, baada ya kupitia CV za makocha waliomba kazi tumeona Badru kutoka Zanzibar atatusaidia, hivyo tukaingia makubaliano ya kuwa kocha mkuu," alisema Kilai.

## Nyimbo za asili zinaibeba jamii

**Na Charles Mandia, SJMC**

NYIMBO za asili bado ni muhimu katika kuhamasisha watu kufanya shughuli mbalimbali za kimaendeleo ikiwamo kilimo, ujenzi na jando, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Elimu wa Kijiji cha Makumbusho, Kinondoni jijini Dar es Salaam, Felix Mulendeu, alisema iko haja ya wananchi kuendelea kuzienzi na kuzilinda nyimbo za kitamaduni kwa vile ni hazina kutoka kwa mababu.

Mulendeu alisema nyimbo hizo ni heshima ya asili ya mtu kwa vile zinasaidia kuburudisha katika shughuli mbalimbali.

"Kiukweli nyimbo za asili ni nyimbo ambazo hutumia ala za muziki za asili ambazo zilitumika na babu zetu kwa kuhamasisha watu, kujumuika pamoja, kuburudika, kulinda na kuendeleza asili," alisema Mulendeu.

Alisema Kijiji cha Makumbusho hutumia Siku ya Makumbusho Duniani kuonyesha nyimbo za tamaduni mbalimbali za jamii zote nchini, vyakula vya asili na shughuli zingine zinazofanywa na makabila nchini.

Debora Mjahiri ni mkazi wa jijini Dar es Salaam aliyekulia mkoani Mara, kwa upande wake aliliambia gazeti hili ngoma za kabila lake zinaitwa Litungu na hutumika katika shughuli za ndoa.

"Vijana wanapopevuka na kwenda jandoni, Litungu inatumika kwa kuelimisha vijana hao kutunza uhusiano ndani ya ndoa, namna gani kumtunza mwanamke na kuhamasisha wanandoa kuishi kwa amani na upendo," alisema.

# Michezo

Alhamisi Februari 11, 2021

Nipashe




BENZEMA: MBIO UBINGWA REAL MADRID BADO NGUMU HABARI UK 22

TUMEWASILI...



Msafara wa wachezaji na viongozi wa Simba ukiwasili mjini Kinshasa, DR Congo tayari kwa mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya AS Vita itakayopigwa nchini humo Ijumaa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# AS VITA YAITISHA SIMBA

●●●Ni wakati ikitua DR Congo, yawaambia wapo kundi la kifo, lakini hawapendi kufa, Msimbazi wajibu...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI kikosi cha Simba kikiwa kimewasili salama mjini Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), tayari kwa mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wenyeji wao, AS Vita wamesema wamejiandaa vema kuhakikisha wanaibuka na ushindi katika mchezo huo wa kwanza wa Kundi A.

AS Vita ambayo mbali na Simba katika kundi lao hilo pia zimo Al Ahly ya Misri na Al-Merrikh ya Sudan, inatarajia kuwakaribisha mabingwa watetezi hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara katika mechi hiyo itakayochezwa Ijumaa nchini humo.

Akizungumza na gazeti hili jana, nahodha wa AS Vita, Jereme Mumbere, alisema wamejipanga kuhakikisha hawapotezi mechi za nyumbani ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

Mumbere alisema timu ambazo ziko katika kundi lao ni nzuri na analiona ndilo kundi la kifo.

"Mimi kama mchezaji, ukiangalia timu zote ambazo tuko nazo ni nzuri, hakuna nafasi ambayo utatoka kirahisi, mimi ninaliita hivyo kundi la kifo, lakini mimi sipendi kufariki ndani ya kundi hilo, tumejiandaa tumalize katika timu mbili za juu, tunapenda tutoke katika timu mbili zitakazofuzu hatua inayofuata, kama timu kwa ujumla tumejiandaa vizuri," alisema nahodha huyo.

**Aliongeza wanatarajia pia kumtumia kiungo wao, Papy Tshishimbi ili kuifahamu vema Simba kwa sababu nyota huyo amecheza nayo katika mechi mbalimbali alipokuwa anaitumikia klabu ya Yanga.**

"Pointi tatu ni lazima nyumbani, pointi tatu nyumbani yaani kwa hali na mali, tumejiandaa vizuri, tunaamini Papy atatusaidia sana kwa uzoefu alionao kwa sababu amecheza mechi nyingi na timu hiyo (Simba), atatuonyesha kupitia uzoefu ambao amepitia, tunajua atatusaidia vizuri," alisema nahodha huyo wa AS Vita.

Aliongeza wamejipanga kufanya vizuri zaidi katika mechi za nyumbani na watakapokwenda kwenye michezo ya ugenini wamelenga kutafuta sare.

"Tumelenga zaidi mechi za nyumbani, tumedhamiria kushinda mechi zote za nyumbani, tutajitahidi mechi zote tutakazocheza nyumbani, tutacheza vizuri, nyumbani hatupotezi," alimaliza nyota huyo.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, aliliambia gazeti hili kuwa wamekwenda DRC kwa kazi moja ya kupambana na kuhakikisha wanavuna matokeo chanya.

"Tuko vizuri na tunakwenda katika kile kinachoitwa vita ya wakubwa, ninawaahidi mashabiki tutahakikisha tunashinda," Manara alisema. Baada ya mchezo wa Jumamosi, Simba itarejea nchini kuendelea na mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara na Februari 23, mwaka huu, itaikaribisha Al Ahly na kati ya Mei 5 na 6 mwaka huu itasafiri kwenda Khartoum kucheza na wenyeji wao, Al-Merrikh.

## NDAYIRAGIJE APIGWA CHINI KUINOA TAIFA STARS

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF) na aliyekuwa Kocha Mkuu wa timu ya Taifa (Taifa Stars), Etienne Ndayiragije, wamefikia uamuzi wa kuvunja mkataba, imefahamika.

Uamuzi huo umekuja wiki mbili baada ya Ndayiragije kushindwa kuivusha Taifa Stars katika hatua ya makundi ilipokuwa ikishiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zilizomalizika nchini Cameroon kwa Morocco kutetea ubingwa.

Taarifa zilizopatikana jijini Dar es Salaam jana zimeeleza TFF imeamua kuachana na kocha huyo raia wa Burundi baada ya kushindwa kufikia malengo ambayo waliwekeana.

"Ni kweli tumeamua kufikia uamuzi huo baada ya kupitia makubaliano ambayo tuliweka wakati tunasaini mkataba, ndio mpira wa miguu ulivyo, ni uamuzi wa kawaida, hata huyo anayekuja naye ataondoka pia," alisema kiongozi mmoja wa TFF.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ndayiragije alisema ni kweli amefikia mwisho wa kibarua cha kuiongoza Taifa Stars baada ya makubaliano ya pamoja na viongozi wa TFF.

"Ndio tumevunja mkataba, sitakuwa na timu hiyo tena," alisema kwa kifupi kocha huyo wa zamani wa Mbao FC ya jijini Mwanza, KMC FC na Azam FC zote za Dar es Salaam.

Mbali na Ndayiragije kuipa Taifa Stars nafasi ya kucheza fainali za CHAN mwaka huu, pia ameiacha timu hiyo ikiwa kwenye hatua ya makundi ya kusaka tiketi ya kushiriki mashindano yajayo ya Kombe la Dunia.

Aliyekuwa kocha wa timu za taifa za vijana, Kim Poulsen, raia wa Denmark anatajwa kurithi mikoba ya Ndayiragije ambaye anatajwa kuongoza kituo kimoja cha soka hapa nchini ambacho kinawamiliki wachezaji mbalimbali wanaoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002